MBOLEA BORA KWA KILIMO ENDELEVU

Mbolea YETU

Tanzania ISSN 2799-2039 **Toleo Na. 03 - Januari - Juni** 2022

Kicheko kwa wakulima: Sh bilioni 150 zatengwa kwa ajili ya ruzuku ya mbolea

uk. 5

Uhamasishaji matumizi sahihi ya mbolea wakonga nyoyo za wakulima

uk. 17

Mwaka mmoja wa Rais Samia: Tasnia ya mbolea yazidi kuimarika

UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI

Dkt. Stephan Eliuth Ngailo
Mkurugenzi Mtendaji

Ujenzi wa viwanda vya mbolea unalenga dhana ya kujitegemea

Kasi ya ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini mwetu inatia moyo katika kuimarisha sekta muhimu ya kilimo ili iweze kutoa mchango wake kwa pato la taifa.

Kwa hakika, ni jambo la kufurahisha kwamba hivi sasa serikali yetu chini ya nahodha wake Rais Samia Suluhu Hassan imepania kuleta mapinduzi ya kilimo katika kuzalisha mazao ya chakula na biashara ili taifa letu liwe na msingi madhubuti wa kujitegemea.

Ujenzi wa viwanda vya mbolea unajikita katika falsafa ya kujitegemea inayolenga kuwakomboa wakulima wa Tanzania kuondokana na uzalishaji duni wa mazao mbalimbali kwenda kwenye uzalishaji wa kisasa wenye tija kwa ngazi ya familia na taifa kwa ujumla wake.

Ni ukweli ulio dhahiri kwamba bila ya kuwakomboa mamilioni ya wakulima wadogo vijijini, nchi yetu itaendelea kuelea kwenye dimbwi la umaskini iwapo idadi hiyo ya wananchi itaachwa nyuma katika maendeleo.

Ni kutokana na ukweli huo ndiyo maana serikali imeweka msukumo mkubwa kwenye ujenzi wa viwanda vya mbolea ili viweze kutosheleza mahitaji ya bidhaa hiyo kwa wakulima badala ya kutegemea uagizaji kutoka nje.

Kilimo cha Tanzania hakiwezi kupiga hatua iwapo taifa litaendelea kutegemea asilimia 90 ya mbolea kutoka nje wakati nchi ina malighafi za kutosha za kuzalisha bidhaa hiyo kwa wingi kwa matumizi ya ndani na usafirishaji nje kwa ajili kupata fedha za kigeni.

Tangu tulipopata uhuru kutoka kwa Waingereza, kauli mbiu yetu iliyoanzishwa na muasisi wa taifa letu Mwl. J.K. Nyerere ilikuwa hakuna jambo lisilowezekana iwapo kila mtu atatimiza wajibu wake. Wajibu wetu sasa ni kuwavutia wawekezaji katika tasnia ya mbolea ili kuchangia jitihada za kuimarisha kilimo chetu.

Ni jambo la faraja kwamba tayari wapo wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kama Misri, Urusi na Slovakia ambao wameonyesha nia ya kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya mbolea nchini mwetu. Pia Benki ya nchi za Kiarabu ya BADEA nayo imeonyesha nia ya kutoa mikopo kwa ajili ya kugharamia usambazaji wa mbolea na ujenzi wa miundo mbinu kama vile maghala, uchanganyaji, upakuaji na ufungashaji.

Lengo kubwa la wawekezaji hao ni kuongeza upatikanaji wa mbolea nchini na hivyo kuleta unafuu wa bei kwa wakulima.

Hamasa ya kitaifa ya ujenzi wa viwanda vya mbolea inaenda sambamba na juhudi za makusudi zilizochukuliwa na Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania ya kuwahamasisha wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea ili kuleta tija kwenye kilimo na kuwaepushakwenye janga la njaa na umaskini na kuwafikisha katika nchi ya ahadi yenye asali na maziwa.

Kwa hakika, hakuna kinachoweza kushindikana zaidi ya juhudi na maarifa.

BODI YA UHARIRI

DANIEL MAARIFA - MWENYEKITI

MATILDA KASANGA - KATIBU

RAYMOND KONGA - MJUMBE

AZIZI MTAMBO - MJUMBE

SALEHE KEJO - MJUMBE

THERESIA SIRIWA - MJUMBE

ALPHA NUHU - MJUMBE

TAHARIRI

Uhamasishaji matumizi sahihi ya mbolea kubadili kilimo Lindi, Mtwara

Katika Miaka 60 ya Uhuru, Tanzania Bara imeshuhudia jitihada nyingi za serikali za kuleta mapinduzi ya kilimo. Zimekuwepo kampeni mbalimbali kama vile Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona na Kilimo Kwanza.

Kampeni hizo zote zililenga kuínua sekta ya kilimo, ambayo kwa asilimia kubwa ndiyo imeajiri mamilioni ya Watanzania waishio vijijini.

Kwa hakika, kwa kiwango kikubwa kampeni hizi zimeleta hamasa miongoni mwa wananchi ya kushiriki kikamilifu katika kubadili kilimo kuwa cha kisasa ili kupambana na adui njaa.

Hata hivyo, jitihada ya kukuza sekta ya kilimo ili isaidie kukuza uchumi wa taifa bado zinaendelea katika karne hii ya 21 ambayo Tanzania inashuhudia kasi kubwa ya ongezeko la watu na mahitaji makubwa ya chakula.

Ni kutokana na ukweli huo Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA) iliandaa Mpango Kazi wa kuhamasisha matumizi ya mbolea katika mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara.

Msukumo wa uhamasishaji wa matumizi ya mbolea katika mikoa hiyo unalenga kupunguza utegemezi wa kuagiza mazao ya nafaka kutoka mikoa ya jirani kwa sababu ya kutegemea zao moja la biashara la korosho.

Uanzishwaji wa mashamba darasa ya kuhamasisha matumizi ya mbolea katika mikoa hiyo utachochea kilimo cha mazao ya chakula na kuchagiza matumizi ya bandari iliyopanuliwa ya Mtwara kupokea shehena za mbolea kwa wingi ili kukuza kilimo katika ukanda wa kusini wa Tanzania.

Ushiriki wa vikundi vya wakulima katika kila hatua ya maandalizi ya mashamba darasa, au mashamba ya mfano ya matumizi ya mbolea, utasaidia kusambaza elimu kwa wakulima wengi na hivyo kuleta tija katika kilimo.

Elimu ya matumizi ya mbolea kwa kuzingatia afya ya udongo, faida za kupima udongo, kanuni za matumizi ya mbolea na dalili mbalimbali za ukosefu wa virutubishi kwenye mimea lazima itolewe kwa wakulima ili wawe na uelewa mpana wa mbinu za kisasa za kilimo katika mazingira yao.

Ni dhahiri kwamba mikoa ya Lindi na Mtwara imejaliwa kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba ambayo ina uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao mengi ya chakula na biashara na kuwa kichocheo cha uchumi wa taifa.

Maendeleo ya kilimo kwa mikoa ya kusini ya Tanzania yatategemea na utashi wa viongozi na ari ya wananchi wenyewe katika kuondokana na umaskini uliokithiri na mapambano dhidi ya janga la njaa.

Inawezekana kabisa kwa mikoa ya Lindi na Mtwara kuzalisha mazao ya chakula na biashara kwa wingi iwapo matumizi ya mbolea yatazingatiwa kama inavyoshauriwa na wataalam.

Kwa mantiki hiyo ni muhimu kwa viongozi wa mikoa ya Lindi na Mtwara wa ngazi zote kusimamia kikamilifu kampeni ya uanzishwaji mashamba darasa ya matumizi ya mbolea vijijini ili wananchi wajifunze mbinu za kilimo bora.

YALIYOMO

Uhamasishaji matumizi sahihi ya mbolea wakonga nyoyo za wakulima *Uk > 5*

Bodi yaainisha mikakati kuhakikisha wakulima wanapata mbolea *Uk > 7*

Massawe aridhika kasi ya ujenzi maabara ya mbolea *Uk > 8*

TFRA yawajengea uwezo wazalishaji mbolea nchini *Uk > 9*

TFRA yajivunia mafanikio utekelezaji bajeti mwaka 2021/22 *Uk > 10*

Neema ya viwanda vya mbolea yazidi kuisogelea Tanzania *Uk > 11*

Matumizi ya chokaa kilimo, jasi yatachochea ufanisi udongo, uzalishaji mazao *Uk > 12*

Wafanyabiashara 135 wa mbolea Kanda ya Ziwa wanolewa *Uk > 16*

Mwaka mmoja wa Rais Samia: Tasnia ya mbolea yazidi kuimarika *Uk > 17*

Orodha ya Mbolea na Visaidizi vya Mbolea vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea, 2009 *Uk > 19*

Kilosa washangilia ujenzi wa kiwanda cha mbolea Dodoma *Uk > 28*

Kicheko kwa wakulima: Sh bilioni 150 zatengwa kwa ruzuku ya mbolea

• Ni kuanzia msimu wa kilimo 2022/2023
• TFRA yapewa jukumu kusajili wafanyabiashara

Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (Mb) akiwasilisha makadirio na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bungeni Jijini Dodoma Mei 3, 2022.

Na **MWANDISHI WETU**

Katika kuhakikisha kwamba sekta ya kilimo inatoa mchango mkubwa kwa uchumi wa taifa, serikali imebuni mkakati madhubuti kwa kutenga shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa mazao yote nchini kwa msimu wa kilimo wa 2022/ 2023.

Kutokana na mkakati huo, Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe (Mb) ameziagiza kampuni na viwanda vyote vya mbolea nchini viwe vimesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kufikia mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu ili kurahisisha utoaji na usimamizi wa ruzuku.

Akiwasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika kikao cha bunge la 13 kilichofanyika jijini Dodoma, Bashe alisema mifuko ya mbolea itakuwa ikiwekwa barcode na lebo ya ruzuku ili kutofautisha na mbolea zitakazoendelea kuuzwa sokoni bila ruzuku.

Alisema kampuni yoyote ambayo haitatekeleza agizo hilo na kukubali kutumia mfumo utakaowekwa na TFRA wa kusimamia na kusajili kampuni na mawakala kwa kuweka eneo la biashara kwenye maduka na ghala zao mikoani, itafutiwa leseni ya biashara.

Waziri Bashe alibainisha kuwa mfumo huo wa mbolea ya ruzuku utawapa kipaumbele wazalishaji wa ndani ili kulinda viwanda vya ndani pamoja na ajira.

"Wizara itaendelea kuwalinda na kuwawezesha wawekezaji wa viwanda vya ndani, kikiwemo kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 za mbolea pamoja na kuwezesha upatikanaji wa vivutio vya uwekezaji kwa kiwanda cha mbolea cha Minjingu ili kuongeza uwezo wake wa kuzalisha tani 300,000 kwa mwaka ifikapo 2023 kutoka tani 100,000 za sasa," alisema Bashe.

Aliwahakikishia wazalishaji wadogo wa mbolea hai *(organic fertiliser)* na chokaa kwamba serikali itaendelea kuwalea, kuwalinda, na kuwahakikishia masoko ili kupunguza gharama za kuagiza aina hiyo ya mbolea kutoka nje ya nchi.

Akizungumzia manufaa ya ziara za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha uhusiano na nchi za Afrika Mashariki, Bashe alisema ni pamoja na kumpata mwekezaji mkubwa wa kiwanda cha mbolea cha ITRAcom Fertilizer Limited kinachojengwa Jijini Dodoma na mwekezaji kutoka nchini Burundi.

Ujenzi wa kiwanda cha Itracom Fertiliser Limited utagharimu dola za Marekani milioni 180 na kinatarajiwa kutoa ajira za kudumu kwa Watanzania zaidi ya 3,000.

Hivi sasa Wizara ya Kilimo inaendelea kuratibu uzalishaji na uingizaji wa mbolea nchini ambapo tani 436,452 za mbolea zimepatikana kwa msimu wa kilimo wa 2021/2022 ikiwa ni asilimia 63 ya mahitaji yote ya mbolea, Tani 274,000 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 43,000 zimezalishwa katika viwanda vya ndani wakati kiasi cha tani 117,900 ni bakaa ya msimu uliopita wa kilimo. Kwa miaka mingi, kilimo kimekuwa ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania kwa kuajiri asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania waishio vijijini.

Tangu taifa hili kubwa la Afrika Mashariki lijipatie uhuru wake kutoka kwa Waingereza miaka 60 iliyopita, sekta hiyo imebaki kuwa mkombozi wa wananchi waishio vijijini.

Ndiyo maana katika miongo sita ya uhuru serikali zote kutoka awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Nyerere zimekuwa zikitilia mkazo kwa kuanzisha kampeni mbalimbali kama vile Kilimo ni Uhai, Kilimo cha Kufa na Kupona na Kilimo Kwanza.

Nia ya kampeni hizo ni kutoa msukumo ili taifa liweze kujitegemea kwa chakula na kuzalisha mazao mbalimbali ya biashara ili kupata fedha za kigeni.

Wakulima wa mpunga wa kikundi cha Tupendane cha Skimu ya Kitere iliyoko Halmashauri ya Mtwara wakijifunza kwa vitendo matumizi sahihi ya mbolea.

Uhamasishaji matumizi sahihi ya mbolea wakonga nyoyo za wakulima

Na **Aziz Mtambo**

Juhudi za Mamlaka za kufuatilia na kutathmini namna mikoa mbalimbali nchini inavyojikita katika kutumia mbolea kwenye shughuli za kilimo zilibaini uwepo wa matumizi hafifu ya pembejeo hiyo kwa mikoa ya kusini mwa Tanzania - Mtwara na Lindi na hivyo kuja na mkakati mahususi wa kuhamasisha wakulima wa mikoa hiyo kutumia mbolea kwa lengo la kuongeza kipato na tija.

Mkakati huo ulikuja na pendekezo la kutumia mashamba darasa ambayo yalishirikisha vikundi vinne vya wakulima vilivyobainishwa kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za mitaa katika mikoa husika na hivyo kufanya ushiriki wa moja kwa moja wa wakulima katika kujifunza kwa vitendo.

Uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea kupitia mashamba darasa umeleta matokeo chanya kwa wakulima kwani wameweza kujifunza kwa nadharia na vitendo kanuni bora za uzalishaji wa zao la mahindi na mpunga kwa kuzingatia matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo anazungumzia ushiriki wa ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara katika kuhamashisha matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wa mikoa hiyo na anasema, mikoa hiyo ililibeba jambo hilo tangu wakati wa maandalizi ya kutenga maeneo, kupima afya ya udongo, kuainisha vikundi vya wakulima vitakavyoshiriki katika shughuli ya uhamasishaji na hata kufikia kilele cha siku ya mkulima kilichofanyika mwezi Aprili katika mikoa hiyo.

Dkt. Ngailo anasema, katika kuhakikisha wakulima wanajikita katika matumizi sahihi ya mbolea wanapaswa kutambua afya ya udongo ya mashamba yao na hivyo kutumia mbolea kulingana na mahitaji ya udongo na mimea.

Katika kuhakikisha hilo linaeleweka kwa wakulima walioshiriki katika mchakato huo TFRA kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Naliendele na wataalamu wa kilimo kutoka ofisi za mikoa ya Lindi na Mtwara kuchukua sampuli za udongo katika maeneo mbalimbali katika mikoa hiyo na kupima katika maabara ya udongo mlingano Tanga na matokeo ya uchambuzi kubainisha upungufu wa virutubisho uliopo katika udongo wa maeneo hayo wenye athari hasi katika uzalishaji wa mazao yaliyofanyiwa uelimishaji.

Anaeleza kuwa, baada ya hatua hiyo mashamba yaliyotumika kwa mafunzo yalibainishwa kwa kushirikiana na vikundi vya wakulima yaliandaliwa kupandwa na kukuzia kwa kutumia mbolea na baadaye wakulima walikwenda kutumia elimu waliyoipata katika mashamba darasa, kwenye mashamba yao binafsi na kupata matokeo chanya.

Dkt Ngailo anasema uelimishaji huo ulitumia kiasi cha tani 5 za mbolea aina ya DAP, Urea, Microp NPKs na NPS kwa mikoa ya Lindi na Mtwara zilizotolewa na wadau wa mbolea kutoka kampuni za Premium Agrochem, OCP Tanzania, YARA Tanzania LTD na ETG na baadaye kila mwanakikundi alipewa mbolea kwa ajili ya kutumia kwenye mashamba yao kwa lengo la kuwavuta wakulima wengine wa karibu kujifunza.

Akizungumza katika moja ya majukumu ya uhamasishaji wa matumizi ya mbolea alipokuwa akikagua mashamba darasa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo anasema, ili mkulima afanikiwe katika shughuli za kilimo ni lazima azingatie kanuni bora za kilimo ikiwa ni pamoja na kuchagua na kuandaa shamba kwa wakati, kupanda mbegu bora zilizothibitishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu nchini (TOSCI), kutumia mbolea sahihi na kwa wakati pamoja na kupalilia na kukuzia kwa wakati lakini pia kutuma viuatilifu sahihi kama kuna magonjwa au wadudu lakini pia kuhifadhi kwa usahihi ili kutunza ubora wake.

Hivyo basi, matumizi ya mbolea ni lazima

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania Dkt. Stephan Ngailo, akitoa maelezo ya matumizi sahihi ya Mbolea Mkoani Lindi.

>>> *Inaendelea Uk. 6*

Mkuu wa Mkoa wa Lindi Bi. Zainab Telack akipata maelezo katika shamba la mfano Wilaya ya Ruangwa wakati wa maadhimisho ya siku ya mkulima katika kampeni ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea.

yaambatane na kanuni bora za kilimo ili kuongeza kipato na tija ambako kutasaidia kupunguza umaskini na kuongeza kipato kitakachotokana na kuvuna kwa wingi kupata chakula na bakaa kuuzwa kwa watu wengine

Dkt. Ngailo anasema, Mamlaka ikishirikiana na halmashauri za mikoa ya Lindi na Mtwara imesimamia vilivyo zoezi hilo ambapo wakulima wamejifunza kwa nadharia na vitendo kanuni bora za uzalishaji wa zao la mahindi na mpunga kwa kuzingatia matumizi sahihi ya mbolea na hivyo kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao hayo.

MAPOKEO YA WAKUU WA MIKOA

Wakuu wa mikoa ya Lindi na Mtwara wakiwa ndio wasimamizi wakuu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa walisimamia kampeni ya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea na kukiri kuwa uhamasishaji huo umefanyika kwa wakati muafaka kutokana na ofisi zao kuwa na lengo la kuwahamasisha wakulima kujikita katika kilimo cha mazao ya chakula na si kilimo cha biashara tu.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi Bi. Zainab Telack aliwaasa wananchi wa mkoa huo kuhakikisha elimu waliyoipata kwa nadharia na vitendo juu ya matumizi sahihi ya mbolea ihamasishwe katika mashamba yao binafsi ili kuona tija ya elimu hiyo na kuongeza kipato chao.

"Mmejionea wenyewe tofauti ya mahindi yaliyopandwa kwa mbolea na yale ambayo hayajatumia mbolea hivyo nawasihi msimu ujao hakikisheni mnatumia mbolea ili kuongeza kipato na tija kwenye shughuli zenu na hii itawapunguzia kutumia nguvu kubwa katika kilimo na kipato kidogo badala yake mtatumia nguvu ndogo kupata matokeo mazuri kwa kutumia mbolea" Telack alikazia.

Mkuu wa Mkoa Telack aliishukuru TFRA kwa juhudi ya kuelimisha umma juu ya matumizi sahihi ya mbolea na kukiri kuwa elimu hiyo itawaondolea wananchi wa maeneo hayo utamaduni wakuhamahama kwa imani kuwa ardhi ikilimwa mara moja inapoteza rutuba na kuwafanya kuhamia katika maeneo ambayo hayajalimwa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dustan Kyobya akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo Brigedia Jenerali Marco E. Gaguti baada ya kupongeza juhudi za TFRA anasema kutokana na umuhimu wa kilimo katika kuchangia ajira, kipato na usalama wa chakula Mkoa wake ulipitisha mikakati ya kuinua uzalishaji wa tija kwenye kilimo.

Anaendelea kusema miongoni mwa mikakati hiyo ni kuongeza wigo wa uzalishaji wa mazao mengine ikiwemo mpunga na kuongeza matumizi ya pembejeo hususani matumizi ya mbolea na mbegu bora.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Kyobya anabainisha kuwa utumiaji wa mbolea mkoani Mtwara upo chini ukilinganisha na mahitaji halisi ya pembejeo hiyo na Mkoa unatumia wastani wa tani 998 za mbolea ambacho ni kiasi kidogo ukilinganisha na lengo la kutumia tani 2,000 kwa mwaka.

Akihamasisha matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima, Kyobya anasema kila mazao yanapovunwa shambani ni dhahiri kwamba virutubisho katika ardhi hiyo hupungua na ili kuirudisha ni sharti mbolea itumike.

Kwa upande wa Katibu wa Kikundi cha Tupendane Bw. Saidi Mtali, katika skimu ya mpunga ya Kitere Kijiji cha Lilido Mkoani Mtwara aliishurkuru TFRA kwa kutoa elimu kwa nadharia na vitendo kwa wanakikundi 15 kwani wameona tija ya kutumia mbolea katika kilimo kwani wameweza kuvuna zaidi ya gunia 30 za mpunga kwa heka.

Akizungumzia changamoto wanazokabiliana nazo Bw Mtali anasema ni pamoja na bei ya mbolea kuwa kubwa na hivyo kushindwa kumudu kununua na kuitumia katika kilimo, pia upatikananji wa mara kwa mara wa elimu ya matumzi sahihi ya mbolea. Pia aliomba Serikali kuwasaidia kuchimba visima vya maji ili kuondokana na changamoto ya maji wanayokumbana nayo katika eneo hilo. Aidha ameiomba TFRA kufanya uhamasishaji huo kwa vipindi vingine viwili vya kilimo ili kuhamasisha zaidi wananchi kutumia mbolea ili kuongeza kipato na tija.

Katika kuendelea kuhakikisha wakulima wanapata tija na kipato hasa katika mazao yote ya chakula na biashara, TFRA itaendelea kufanya uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea katika mikoa hii ya kusini (Lindi na Mtwara) ili kuongeza matumizi ya mbolea kwa msimu ujao wa kilimo lakini pia kuendelea kusisitiza matumizi sahihi kw nchi nzima kupitia ofisi zake za kanda kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa katika maeneo husika.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dustan Kyobya, akizungumza kwenye kilele cha siku ya mkulima Mkoani Mtwara.

Bodi yaainisha mikakati kuhakikisha wakulima wanapata mbolea

Na **MWANDISHI WETU**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Prof. Anthony Mshandete ameweka wazi mikakati mahususi ya kuhakikisha wakulima nchini wanapata mbolea bora.

Alieleza mikakati hiyo Aprili 29, 2022 wakati wa ziara ya wajumbe wa Bodi ya TFRA pamoja na watendaji wa mamlaka hiyo katika eneo kinapojengwa kiwanda cha mbolea cha Itracom Limited, ziara iliyolenga kujionea hatua na maendeleo ya ujenzi wa kiwanda kinachotarajia kuanza na uzalishaji wa mbolea ifikapo mwezi Julai 2022.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Prof. Anthony Mshandete (wa tatu kutoka kushoto) akiongea wakati ya ziara ya kujionea maendeleo ya ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha ITRACOM Limited kinachotarajiwa kuanza na uzalishaji wa tani 600000 za mbolea ifikapo mwezi Julai 2022.

Baadhi ya mitambo iliyofungwa kwenye kiwanda cha mbolea cha ITRACOM Limited kinachojengwa jijini Dodoma

Akieleza mikakati hiyo, Prof. Mshandete alisema mkakati wa kwanza ni kuhakisha mbolea inayozalishwa inakuwa na ubora na viwango vinavyokubalika nchini. Alisema wananchi wakiona ubora wa mbolea inayozalishwa na kiwanda hicho itakuwa rahisi kwa kiwanda kujitangaza na mbolea itauzika kiurahisi.

Akielezea mkakati wa pili Prof. Mshandete alisema ni uongozi wa kiwanda kuwa na mkakati wa mawasiliano kwa ajili ya kutangaza aina ya mbolea itakayokuwa ikizalishwa na kiwanda hicho yenye mchanganyiko wa samadi na madini mengine kama phosphate na chokaa tofauti na aina zilizozoeleka na wakulima nchini.

Prof. Mshandete alisema kutokana na ukweli kwamba mbolea inayozalishwa kiwandani hapo kuwa mpya kwenye soko la ndani elimu kuhusu ubora wa mbolea hiyo unapaswa kutolewa ili wananchi waweze kuifahamu na kuwa na utayari wa kuitumia na hivyo kupunguza changamoto ya upatikanaji wa mbolea nchini.

Zaidi, Prof. Mshandete aliwataka wasimamizi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer LTD kuwa na hari (aggressiveness) katika kutangaza bidhaa na kuwashauri kushiriki katika maadhimisho ya siku ya mbolea yanayotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu ili kuwapa fursa ya kutangaza bidhaa zake.

Akizungumzia suala la upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea kiwandani hapo Prof. Mshandete alisema kutatokana na namna nzuri ya kutangaza uwepo wa kiwanda hicho pamoja na kutangaza malighafi zinazotumika katika uzalishaji kutakakofanywa na mwekezaji huyo.

Prof. Mshandete pia ametoa wito kwa mwekezaji Itracom Fertilizer LTD kutosita kuishirikisha TFRA na mamlaka nyingine za serikali pindi wanapokutana na changamoto wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Akizungumza kwa upande wa mwekezaji, Dkt. Ntukamazina Nepomuscene Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu wa Itracom Fertilizer LTD alisema ujenzi wa kiwanda upo katika hatua nzuri ambapo mitambo imeshaanza kufungwa tayari kuanza uzalishaji ifikapo Julai 2022.

Aliongeza kuwa, tayari kiasi kikubwa cha samadi kimepatikana na kimefikishwa kiwandani hapo kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa mbolea hiyo.

Uwekezaji huo unaotarajiwa kugharimu kiasi cha dola za kimarekani Milioni 180 ni matokeo ya ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan nchini Burundi na kueleza fursa za uwekezaji zilizopo nchini na kumpata mwekezaji wa kiwanda cha Itracom Fertilizers Limited.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Andrew Massawe (wa tatu kutoka kushoto) akisikiliza maelezo ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Jengo la Maabara ya Mbolea linalojengwa katika eneo la kilimo III Temeke, jijini Dar es Salaam.

Massawe aridhika kasi ya ujenzi maabara ya mbolea

Na **MWANDISHI WETU**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Andrew Massawe, ameridhishwa na ubora na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa maabara ya kimataifa ya mbolea, mradi ambao unatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

Ujenzi huo hadi mwezi Mei, 2022 umefikia asilimia 60 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai mwaka 2022.

Bw. Massawe alitoa pongezi hizo hivi karibuni alipotembelea ofisi za Mamlaka hiyo kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo wa maabara pamoja na utekelezaji wa maelekezo aliyotoa mwezi Novemba mwaka jana kuhusu ujenzi wa maabara hiyo eneo la Kilimo III, Temeke, jijini Dar es Salaam.

Pamoja na hayo, alielekeza Menejimenti ya TFRA kuangalia uwezekano wa kuongeza idadi ya ghorofa ili kuweza kuwahudumia wateja wengi wenye mahitaji mbalimbali yanayohusiana na kilimo kwa kuwa na taasisi zingine ndani ya jengo moja.

Akizungumzia maendeleo ya mradi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi Bw. Joseph Charos alieleza kuwa ujenzi umefikia asilimia 60 ambapo upigaji plasta kwenye kuta katika ghorofa ya chini (ground floor) ikiwa ni pamoja na uwekaji wa miundombinu ya awali ya umeme na maji (First fix services) umekamilika na kuongeza kuwa umwagaji wa zege (slab) la sakafu ya pili pia umekamilika.

Kufuatia maelekezo yaliyoyatolewa na

> **Ujenzi umefikia** asilimia 60 ambapo upigaji plasta kwenye kuta katika ghorofa ya chini ikiwa ni pamoja na uwekaji wa miundombinu ya awali ya umeme na maji (First fix services) umekamilika

Katibu Mkuu Massawe ya kulifanya jengo hilo kuwa kitovu cha taarifa, huduma na habari zote zinazohusiana na mbolea nchini (fertilizer one stop centre), Mamlaka ilieleza kupokea maelekezo hayo na kuanza kuyafanyia kazi na hivyo kuifanya maabara kuwa ya kisasa na ya kuvutia na kuwa ni kituo cha ubora kuhusu masuala yote yanayohusu mbolea (Fertilizer Centre of Excellence).

Pamoja na hayo Bw. Charos, alieleza kuwa Menejimenti imeendelea kushirikiana na Mshauri Elekezi kuona namna inavyoweza kuboresha muonekeno wa jengo (State of Art), hususan katika ghorofa mbili zinazotarajiwa kuendelea kujengwa.

Aidha, kuhusu kuifanya maabara hiyo kuwa kitivo cha masuala yote ya mbolea (Fertilizer One Stop Centre), Charos amesema Mamlaka itashirikiana na taasisi nyingine zinazojihusisha na shughuli za mbolea kutimiza azma hiyo.

Akizungumzia gharama zilizotumika katika utekelezaji wa mradi huo, Charos alisema kufikia Machi 30, 2022 jumla ya Shilingi 746,016,267.43 zimetumika kwa ajili ya manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali kwenye eneo la ujenzi.

Ujenzi wa maabara ya kisasa ya mbolea nchini ni suala muhimu kwa Mamlaka kwani itaondoa changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa majibu ya vipimo vya mbolea kwa haraka.

TFRA yawajengea uwezo wazalishaji mbolea nchini

Na **MWANDISHI WETU**

Timu ya wataalam kutoka Makao Makuu ya Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA) Februari 15, 2022 iliendesha mafunzo mkoani Arusha ya kuwajengea uwezo wa kimtaji na kitekinolojia wazalishaji wadogo wa mbolea ili waendeleze shughuli zao kwa ufanisi.

Wataalam hao waliongozwa na Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Mazingira, Stephenson Ngoda kwa lengo la kuwaelimisha wadau ili wazifahamu sheria na miongozo mbalimbali inayotumiwa na TFRA katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake.

Viongozi wa TFRA Makao Makuu pamoja na ofisi zake za kanda wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba wanawafikia wadau wao na kuwapa elimu ya uzalishaji na biashara ya mbolea.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Ngoda alisema kwamba agenda kubwa kitaifa ni kuongeza uzalishaji wa ndani wa mbolea ili kukidhi mahitaji ya wakulima kwa kuwa malighafi za kuuzalisha bidhaa hiyo zinapatikana nchini kwa wingi.

Alisema mafunzo hayo yana umuhimu wa pekee katika kuwawezesha wazalishaji wa ndani kuzalisha mbolea bora ili kupunguza uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ambao umesababisha uhaba na kupanda kwa bei kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Uviko 19.

"Wazalishaji wengi wamekuwa na changamoto za miundombinu duni na mitaji hivyo kikao hiki kimewakutanisha wazalishaji na watoa huduma za kifedha ili kuwawezesha kupata mitaji na teknolojia bora itakayowawezesha kuzalisha kwa tija," Ngoda alisema.

Katika mafunzo hayo, mwezeshaji kutoka Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO), Nina Nchimbi, aliwataka wazalishaji wa mbolea kutafuta taarifa sahihi zinazohusiana na shughuli zao ili kuongeza tija katika uwekezaji wao na kupata ufumbuzi wa changamoto za mitaji zinazowakabili.

Alisema SIDO ipo kwa ajili ya kuwasaidia kuwapa ushauri katika uanzishaji wa viwanda vyao na kuwarahisishia usajili wa bidhaa wanazozalisha ili ziweze kuthibitishwa na Shirika la Viwango (TBS).

Pia walikuwepo wawezeshaji wengine kutoka benki za NMB na CRDB, PASS, EFTA ambapo wote walieleza misaada ya kitaalamu inayotolewa kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuandika maandiko ya biashara inayowawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha, kuwakopesha vifaa au mitambo, na kuwapa ushauri wa kitaalam katika uzalishaji wa mbolea ili kukidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Ofisi za TFRA za Kanda zimeendelea na juhudi za kuwaelimisha wadau wa mbolea katika nyanja mbalimbali ikiwemo uhifadhi bora wa mbolea, sheria pamoja na mfumo wa Taarifa za Mbolea (FIS). .

Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Mazingira wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Stephenson Ngoda akiongea jambo wakati wa semina kwa wazalishaji wadogo wa mbolea nchini iliyoandaliwa na Mamlaka hiyo kwa lengo la kuwaongezea uwezo ili wazalishe kwa viwango vinavyokubalika na kuwaongezea tija.

Akitoa taarifa ya mafunzo yaliyofanyika katika Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kaimu Meneja wa Kanda hiyo, Michael Sanga, alisema mafunzo ya uhifadhi bora wa mbolea, sheria pamoja na mfumo wa FIS yalitolewa kwa wafanyabisahara wa mbolea 419 kutoka katika mikoa ya Mbeya (141), Iringa (82), Ruvuma (123), na Njombe (73).

Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 14 ikilinganishwa na wafanyabiashara 367 waliopata mafunzo mwaka 2021. Ongezeko hilo, kwa mujibu wa Sanga, linatokana na ushirikiano kati ya Halmashauri za Wilaya na ofisi ya kanda pamoja na kuongezeka kwa nguvu kazi katika ofisi hiyo.

Kaimu Meneja wa Kanda ya Ziwa, Khanafi Mohamed, alisema mafunzo kwa wafanyabiashara wa mbolea 345 yalitolewa katika mikoa ya Mwanza (116), Mara (55), Simiyu (31), Shinyanga (56), Geita (73) na Kagera (14). Hali kadhalika, mafunzo ya utunzaji na matumizi ya mbolea yalitolewa kwa wanafunzi 150 wa MATI Ukiriguru.

Naye Kaimu Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Gothard Liampawe, alieleza kuwa mafunzo ya utunzaji, uhifadhi wa mbolea pamoja na usajili kupitia mfumo wa FIS yalitolewa kwa wafanyabiashara wa mbolea wapatao 241 kutoka katika mikoa ya Arusha (196) na Manyara (45).

Utoaji wa mafunzo unakwenda sambamba na shughuli ya ukaguzi wa mbolea katika kuhakikisha udhibiti wake unafanyika kikamilifu ambapo katika robo ya tatu, ofisi ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) ilifanya ukaguzi kwa wafanyabiashara wa mbolea 493 kutoka katika mikoa ya Mbeya (78), Njombe (43), Ruvuma (145), Iringa (41), Katavi (15), Songwe (105) na Rukwa (66). Hili ni ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na wafanyabiashara 457 waliokaguliwa mwaka jana kipindi kama hiki kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Wakati huohuo, taarifa kutoka Kanda ya Ziwa zinaeleza kuwa kwa kipindi cha Januari hadi Machi, 2022 ofisi hiyo ilikagua wafanyabiashara wa mbolea 119 katika mikoa ya Simiyu (19), Mwanza (40) na Mara (60). Vilevile ilifanya ukaguzi wa maghala na sehemu za kuhifadhia mbolea zipatazo 122 -- Mwanza (40), Simiyu (20) na Mara (62). Idadi ya wafanyabiashara wa mbolea waliokaguliwa imeongezeka kwa asilimia 128.8 ikilinganishwa na wafanyabiashara 52 waliokaguliwa mwaka jana katika kipindi kama hicho.

Kwa upande wa taarifa za ukaguzi kwa Kanda ya Kaskazini, kati ya Januari hadi Machi, 2022 ofisi ya kanda hiyo ilikagua wafanyabiashara wa mbolea 158 katika mikoa ya Tanga (30), Arusha (67), Kilimanjaro (61) na viwanda vya mbolea viwili. Ukaguzi huo uliambatana na ukaguzi wa maghala ya kuhifadhia mbolea. Wafanyabiashara waliokaguliwa ni sawa na ongezeko la asilimia 1.2 ikilinganishwa na Idadi ya wafanyabiashara 156 waliokaguliwa mwaka jana katika kipindi kama hicho.

Utoaji wa mafunzo kwa wadau unawasaidia kutokiuka sheria na maelekezo wanayopewa na TFRA.

Mwonekano wa jengo la maabara litakapokamilika. Maabara hii itaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya TFRA. Vilevile, inategemewa kutumiwa na nchi jirani zinazotumia bandari za Tanzania kama vile Malawi, Zambia, DRC, Burundi na Rwanda.

TFRA yajivunia mafanikio utekelezaji bajeti mwaka 2021/22

Na **Theresia Siriwa**

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) tangu kuanzishwa kwake mwaka 2012 inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea Na. 9 ya Mwaka 2009. Aidha majukumu hayo yanatekelezwa kwa kufuata Mpango Mkakati wa TFRA wa miaka Mitano (2021/22-2025/26). Majukumu hayo yamelenga kufanikisha malengo ya Kimkakati ya Kitaifa ikiwemo Mpango wa Kitaifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano awamu ya tatu, Program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ASDP II na Ilani ya chama Tawala (2020 - 2025).

Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, hadi kufikia mwezi Machi, 2022 TFRA imefanikiwa kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa asilimia 92.5% ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana ambapo utekelezaji wake ulikuwa asilimia (87.4%). Mafanikio haya yametokana na ongezeko la watumishi na mfumo wa kielekroniki wa taarifa za mbolea (FIS) ambao umewezesha wateja kupatiwa huduma kwa njia ya mtandao, hivyo kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwemo usajili wa wafanyabiashara, utoaji wa vibali vya uingizaji na utoaji mbolea

Katika kuhakikisha wadau wa kilimo wanapata mbolea kwa wakati na yenye ubora unaotakiwa mwaka wa fedha 2021/22, TFRA makao makuu, pamoja na ofisi zake za kanda ilifanikiwa kufanya ukaguzi wa mbolea kwa wafanyabiashara 3,276 katika mikoa ya; Dar es Salaam (150), Pwani (231), Morogoro (297), Lindi (66), Mtwara (76), Tabora (106), Kigoma (90), Njombe (177), Mbeya (173), Ruvuma (216), Iringa (95), Katavi (72), Songwe (230), Rukwa (144), Mwanza (128), Simiyu (53), Mara (89), Shinyanga (41), Geita (33), Kagera (27), Tanga (97), Manyara (108) Arusha (129) Kilimanjaro (145), Singida (144) na Dodoma (146). Ukaguzi kwa wafanyabiashara 3,276, idadi hii ni ongezeko la asilimia (49.6%) ya idadi ya wafanyabiashara 2,189 waliokaguliwa mwaka 2020/21.

Mamlaka ilitoa mafunzo ya utunzaji, uhifadhi wa mbolea, sheria zinazosimamia tasnia ya mbolea pamoja na usajili kupitia mfumo wa FIS ambapo wafanyabiashara wa mbolea 3,777 kutoka katika mikoa ya Dodoma (81), Siniga (73), Mwanza (116), Mara (55), Simiyu (31), Shinyanga (56), Geita (73), Kagera (14), Songwe (182), Rukwa (46), Katavi (40), Mbeya (369), Ruvuma (345), Njombe (335), Iringa (251), Arusha (273), Kilimanjaro (78), Tanga (60), Manyara (71), Mtwara (160), Lindi (175), Pwani (74) na Morogoro (819). Idadi ya wafanyabiashara walipopatiwa mafunzo katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022 ni ongezeko la asilimia (49.8%) ya idadi ya wafanyabiashara na wadau wa mbolea 2521 waliopatiwa mafunzo mwaka jana (2020/21).

Mamlaka imeanza ujenzi wa maabara ya kupima ubora wa mbolea, ambapo hadi kufikia Machi, 2022 ujenzi wa maabara hiyo umefikia asilimia 60. Maabara inategemea kuanza kutoa huduma mwezi octoba 2022, ambapo kukamilika kwa maabara kutaiwezesha TFRA kutoa huduma za upimaji wa mbolea kwa ufanisi zaidi.

Katika kuhakikisha kuna upatikanaji wa takwimu sahihi za mbolea, utoaji huduma kwa ufanisi, Mamlaka kwa kushirikiana na wakala wa mtandao serikalini (E-Government) imeendelea kuboresha mfumo wa FIS ambao umerahisisha huduma za utoaji leseni kwa wafanyabiashara wa mbolea, vibali vya kuingiza na kusafirisha mbolea. Huduma hizo kwa sasa zinatolewa kwa siku moja ukilinganisha na hapo awali kabla ya mfumo ilikuwa inachukua zaidi ya siku saba (7).

Vilevile katika mwaka wa fedha 2021/22 TFRA imehamasisha matumiz sahihi ya mbolea kwa wadau wa kilimo kwenye Siku ya Mbolea Duniani ambayo yameadhimishwa mkoani Ruvuma (Songea), pia ilishiriki kwenye maadhimisho ya kitaifa ya wafanyabiashara (Sabasaba). Aidha, kupitia kampeni hiyo, TFRA imehamasisha matumizi sahihi ya mbolea katika mikoa ya Mtwara na Lindi, ambapo Mashamba darasa manne (4) katika Halmashauri za Mtama, Ruangwa, Mtwara na Masasi yalianzishwa na zaidi ya wakulima 5000 wamepata elimu kupitia mashamba hayo.

Pia Mamlaka imefanikiwa kuanzisha ofisi mpya ya Kanda ya Kati mkoani Tabora, ambayo inahudumia mikoa ya Tabora, Dodoma na Singida. Hivyo, TFRA kwa sasa ina jumla ya ofisi za kanda nne (4), ambazo ni kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Ziwa (Mwanza) na kanda ya Kati (Tabora).

Mafanikio haya ni kutokana na jitihada za TFRA na ushirikiano uliopo kati ya wadau mbalimbali katika sekta ya kilimo ikiwemo Wizara mama, Watendaji kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na sekta binafsi. TFRA itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika sekta ya kilimo ili kufikia Malengo iliyojiwekea katika mwaka wa fedha ujao wa 2022/23 kwa lengo la kuhakikisha mbolea bora inamfikia mkulima kwa wakati na kwa bei nafuu.

Mafanikio haya ni kutokana na jitihada za TFRA na ushirikiano uliopo kati ya wadau mbalimbali katika sekta ya kilimo ikiwemo Wizara mama, watendaji kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na sekta binafsi

Neema ya viwanda vya mbolea yazidi kuisogelea Tanzania

- **Lindi, Mtwara kunufaika**

Mwekezaji kutoka Misri ameonyesha nia ya kujenga viwanda viwili nchini vya kuzalisha mbolea ya aina mbili katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam au Pwani.

Hii ni kwa mujibu wa mazungumzo yaliyofanyika Januari mwaka huu kati ya mwekezaji huyo na Mamlaka ya Udhibiti Mbolea Tanzania (TFRA) na Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Kaimu Meneja Uzalishaji wa Ndani wa TFRA, Stephanson Ngoda, aliyehudhuria mazungumzo na mwekezaji huyo, amesema kiwanda cha kwanza kinachotarajiwa kujengwa Lindi au Mtwara kitakuwa kinazalisha mbolea aina ya Urea wakati kiwanda cha pili kinachotarajiwa kujengwa mkoa wa Dar es Salaam au Pwani kitakuwa kikizalisha mbolea ya ***fertilizer blending***.

Katika hatua nyingine Ngoda amesema mazungumzo yaliyofanyika Machi 16 mwaka huu kwa njia ya mtandao, mwekezaji wa kampuni ya URACHEMI na URAKALI kutoka Urusi ameonyesha nia ya kuwekeza kwenye viwanda vya kuchanganya mbolea kwa kushirikiana na Kampuni la Mbolea Tanzania (TFC).

"Mwekezaji huyo alipewa utaratibu wa kufuata ili aweze kuanza hatua ya kuwekeza katika tasnia ya mbolea hapa nchini," amesema Ngoda.

Ngoda amesema katika kikao cha tatu kilichofanyika Machi 22, 2022 benki ya nchi za Kiarabu ya BADEA ilionyesha nia ya kutoa mikopo kwa ajili ya kugharamia usambazaji wa mbolea na ujenzi wa miundo mbinu kama maghala, uchanganyaji, upakuaji na ufungashaji.

Wawakilishi wa benki hiyo pia walionyesha nia ya kuwatumia wabia wao, ambao ni wazalishaji wakubwa wa mbolea, ili kuwekeza katika uingizaji wa mbolea nchini kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa bidhaa hiyo ili kuleta unafuu wa bei.

Kwenye kikao cha nne kilichofanyika Mei 27 mwaka huu, Ngoda amesema wawakilishi wa mwekezaji wa Kiwanda cha Rokosan/ROKOVIA walibadilishana uzoefu na mikakati ya kupata malighafi na wateja na wadau wa kiwanda cha machinjio ya kisasa,TANCHOICE, kampuni ya uzalisahji wa sukari ya Azam, Tume ya Ushirika, Bodi ya Sukari, na wawakilishi wa kampuni ya ROKOSUN/ROKOVI nchini ambao ni SELFINA na Kahama Oil Millers LTD (KOM).

Mwekezaji wa Rokoson/ROKOVIA pia alifanya kongamano la kitaalamu Machi 2022 kujadili na kuwaelewesha wadau jinsi bidhaa za mbolea ya kampuni za Rokoson/ROKOVIA zinavyofanya kazi sehemu mbalimbali duniani na manufaa yake kwenye uzalishaji na kutunza mazingira.

Ngoda amesema mwekezaji huyo anategemea kuwekeza kiasi cha Euro 40 million (Tshs. 97.8 Bn) na kuajiri watu 150 ambapo baada ya kukamilika miradi ajira 1,000 zitapatikana kwa kuwa na mtandao wa matawi 26 ya usambazaji nchi nzima.

Kwa mujibu wa mapitio yaliyofanyika Mei mwaka huu, viwanda vya mbolea vilivyopo ambavyo vinaendelea kuzalisha mbolea ni 16. Viwanda hivyo vimegawanyika katika makundi makuu mawili: vinavyozalisha mbolea na vile vinavyozalisha visaidizi vya mbolea

Kwa mujibu wa mapitio yaliyofanyika Mei mwaka huu, viwanda vya mbolea vilivyopo ambavyo vinaendelea kuzalisha mbolea ni 16. Viwanda hivyo vimegawanyika katika makundi makuu mawili: vinavyozalisha mbolea na vile vinavyozalisha visaidizi vya mbolea.

Viwanda vinavyozalisha mbolea huzalisha mbolea ya aina mbili ambazo ni mbolea iliyo katika hali ya yabisi au ngumu na mbolea iliyo katika hali ya kimiminika au unga ambapo wakati wa kuwekwa shambani huchanganywa na maji na kuwekwa katika majani ya mmea. Mbolea hizi hujulikana kama foliar fertilizers.

Kwa sasa idadi ya viwanda vinavyozalisha mbolea nchini ni 13 ambapo kati ya viwanda hivyo, viwanda vitano vina miundo mbinu na mitambo yenye kiwango cha kuitwa kiwanda. Kiwanda cha Minjingu ndicho kikubwa kuliko vyote kikifuatiwa na Yara, Keen Feeders , ETG inputs na Farm Access Company Limited.

Viwanda vingine vitano vya Sianga Agro Traders, Mtali Agrotraders, Isacha Feeders, Amka Feeders na Kehela Group havina miundo mbinu na mitambo ya kisasa ya kuzalishia mbolea, kwa mujibu wa Ngoda.

"Viwanda hivi vimekuwa vikizalisha kwa kutumia teknolojia duni ya madumu ya maji ya Simtank ambapo wanachanganya mbolea kwa kutumia pump/mashine ndogo ndogo na wengi wanachanganya kwa kutumia mikono bila mashine/pampu," anaeleza Ngoda.

Anasema viwanda vingine vitatu vya Guavay Company Limited , Farm Times na Mabwepande Composite Manure vina miundo mbinu na mitambo ya "kiwango cha kuridhisha kuitwa kiwanda" na vimejikita katika kuzalisha mbolea ya asili (organic fertilizers).

Idadi ya viwanda vinavyozalisha visaidizi vya mbolea ni vitatu na vinatofautiana kwa ukubwa kulingana na miundombinu na mitambo ya kuzalishia mbolea. Kulingana na kiwango cha visaidizi vya mbolea vinavyozalishwa, kiwanda cha ABM Equipment Limited ni kikubwa kikifuatiwa na Dodoma Cement na HSSL.

Ujenzi wa kiwanda cha ITRACOM kilichopo Jijini Dodoma umefikia asilimia 80 ukiwemo uzio, majengo ya ofisi, maghala na majengo ya kiwanda. Ununuzi wa mitambo ya kuzalishia mbolea ambayo tayari imewasili katika eneo la kiwanda umefikia asilimia 90.

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbolea unaongezeka nchini, TFRA imeendelea kuwajengea uwezo wazalishaji wadogo wa mbolea za maji (foliar fertilizers) ambao wamekuwa wakitumia miundombinu na mitambo hafifu, hali iliyosababisha kuwepo kwa mbolea zisizo na ubora zinazozalishwa na viwanda hivyo.

Matumizi ya chokaa kilimo, jasi yatachochea ufanisi udongo, uzalishaji mazao

Na Raymond Konga

Mimea inaweza kustawi au kutostawi katika udongo wenye sifa mbalimbali za kikemia ambazo huwa na matokeo chanya au athari hasi kutegemeana na hali husika.

Sifa kubwa ya kikemia katika udongo ni pH ambayo ikiwa chini au juu zaidi huleta athari hasi katika ukuaji wa mimea ya aina nyingi. pH inayokubalika kwa ukuaji wa mimea mingi ni ya kati/huru.

Iwapo itatokea sifa hiyo ya kikemia kutoendana na mahitaji ya mazao yanayotarajiwa kuzalishwa, hali hiyo hutakiwa kurekebishwa kwa kutumia chokaa kilimo au jasi.

pH ya udongo ni nini?

pH ya udongo ni hali ya udongo kuwa na tindikali (acidity), magadi (alkalinity) au huru (neutral).

Umuhimu wa kipimo cha pH ya udongo (soil pH) katika kilimo

Kipimo cha pH ya udongo hutumika kama kiashiria kikuu ambacho huonyesha tindikali au magadi katika udongo. Kipimo hiki hupima viwango kuanzia 0 hadi 14, ambapo 0 hadi 6 ni tindikali, 7 pH huru na 8 hadi 14 ni magadi, mchoro wa kielelezo Na. 1 unafafanua.

Kielelezo Na. 1



pH 6.0 hadi 7.0 katika udongo ni kiwango ambacho mazao mengi ya kilimo hustawi vizuri. Kuna baadhi ya mazao hustawi vizuri pia katika pH ya kiwango cha chini ya 6 hadi 5.5 au kiwango cha juu pH ya 7 hadi 8. Aidha, mimea hutofautiana jinsi inavyoathiriwa na kiwango cha chini au cha juu cha pH ya udongo.

Athari za tindikali na magadi katika kilimo

Hali ya tindikali na magadi ni sifa za msingi za udongo kama unafaa kwa kilimo, na ni moja ya mambo muhimu yanayoathiri rutuba ya udongo.

Namna tindikali na magadi zinavyoathiri rutuba ya udongo

Katika udongo wenye tindikali na magadi upatikanaji wa virutubishi muhimu vya mimea huathiriwa kwasababu za kikemikali ambazo huathiri ufanisi wa virutubishi katika ukuaji mimea, Kielelezo Na. 2 kinaonyesha uhusiano uliopo kati ya pH ya udongo na upatikanaji wa virutubishi muhimu vya mimea.

Kielelezo Na. 2



Chanzo: www.agrobest.com

Kuathirika kwa shughuli za viumbe hai (soil microorganisms) kwenye udongo

Kwa kawaidia viumbe hai hupendelea kuishi kwenye udongo wenye pH ya 6.5 hadi 7.5, hivyo tindikali nyingi au magadi mengi kwenye udongo huathiri shughuli za viumbe hai ambapo huathiri ubadilikaji na usambazaji wa nitrojeni na virutubishi vingine.

Udongo wenye tindikali nyingi unakabiliwa na upatikanaji wa madini yenye sumu (kama Aluminium (Al^{3+}) na Manganese) na kwenye udongo wenye magadi kwa wingi husababisha mkusanyiko wa chumvi pamoja na madini ya sodium carbonates ambayo huchangia kuharibu muundo wa udongo hivyo kuathiri uotaji, ukuaji wa mizizi na mazao kwa ujumla.

Kwa nini udongo unakuwa na viwango tofauti vya pH?

Baadhi ya sababu zinazofanya udongo kuwa na viwango tofauti vya pH ni pamoja na;-

i. Uwepo wa mvua nyingi kwa muda mrefu, ambazo huosha virutubishi vya msingi kwenye udongo kama vile potasiamu, kalisiumu na magnesiamu na kuacha haidrojeni ioni (H+), aluminiumu na manganese ambayo husababisha tindikali.
ii. Matumizi yasiyo sahihi ya mbolea ambapo huchujika na kusababisha haidrojeni ioni (H^+) ambayo huongeza tindikali kwenye udongo.
iii. Kutofanya hifadhi ya udongo, na uwekaji mbolea zenye virutubishi linganifu.
iv. Asili ya udongo wenyewe (mineralogical composition).

Namna ya kupunguza athari za pH ya udongo

Tindikali nyingi na magadi kwa wingi kwenye udongo hurekebishwa kwa kutumia visaidizi vya mbolea (fertilizer supplements) ambavyo vinajumuisha chokaa kilimo kwa udongo wenye tindikali na jasi au madini ya salfa kwenye udongo wenye magadi.

Chokaa kilimo

Chokaa Kilimo (Agricultural limestone) ni mchanganyiko wa madini ya asili ya miamba yenye virutubishi vya kalisiumu (calcium) na magnesiamu (magnesium) kwa ajili ya kupandisha pH kwenye udongo wenye tindikali (acidic soil) ili ukaribie pH huru (neutral)

Aina za chokaa kilimo

i. AgLime (Calcium Carbonate ($CaCO_3$)) au Calcium Oxide (CaO) ambayo pia inaitwa Calcitic limes
ii. Dolomitic Lime (Calcium Carbonate and Magnesium Carbonate ($MgCO_3$)). Hii ina virutubisho vya Kalisiumu na Magnesiamu.

Umuhimu wa chokaa kilimo katika udongo wa kilimo

- Hutoa virutubishi vya kalisiumu na/ au magnesiam
- Husaidia kupandisha pH kwenye udongo wenye tindikali ili kufikia lengo ya pH huru.
- Kupunguza uwezekano wa uyeyukaji wa madini yenye sumu ya Aluminium (Al^{3+}) na manganese ambayo huathiri ukuaji wa mizizi ya mmea.
- Huongeza uwezo wa mmea kuchukua virutubisho vya nitrojeni, fosiforasi, potashi na salfa kutoka kwenye udongo

Jasi

Jasi (Agricultural gypsum) ni mchanganyiko wa madini yenye virutubishi vya kalisiumu na salfa (sulphur). Jasi husaidia kuboresha udongo (soil conditioner) wenye magadi (alkali or sodic soils) kwa kupunguza wingi wa madini ya sodium kwenye udongo hivyo kusaidia kushusha kiwango cha pH kwenye udongo.

Aina ya jasi

- Agricultural Gypsum (Calcium Sulphate ($CaSO_4.2H_2O$))



Chanzo: TARI

Umuhimu wa jasi katika udongo wa kilimo

- Hutoa virutubishi vya Kalisium na Salfa kwenye mimea
- Husaidia kupunguza kiwango cha chumvi (sodiam) kwenye udongo hivyo husaidia kupunguza pH ya udongo
- Hurekebisha udongo ulioshikamana yaani udongo mfinyanzi (clay soil) kwa kuboresha muundo wa udongo ili uweze kuruhusu mizizi, maji na hewa kupenya na uotaji wa mbegu.
- Kupunguza uwezekano wa uyeyukaji wa madini yenye sumu ya sodium carbonate ambayo huathiri ukuaji wa mizizi ya mmea.

Uwekaji wa chokaa kilimo, jasi

Matumizi ya chokaa kilimo na jasi lazima yazingatie afya ya udongo ili kutambua kama kiwango cha pH pamoja na virutubishi vipo kwa kiasi gani, kujua aina na kiasi kinachotakiwa cha kuwekwa shambani kwa mwaka ili kuongeza au kupunguza pH kwenye udongo, pia hutegemea aina ya zao litakalopandwa.

Uwekaji wa chokaa kilimo au magadi hufanyika kabla au wakati wa kupanda mazao. Huwekwa kwa kuchanganywa na udongo au kuwekwa katika mashimo yatakayo tumika kupanda mazao. Aidha, wakati wa kuweka ni muhimu kuzingatia uwezo wa kuyeyuka (solubility) kwa chokaa kilimo au jasi katika ardhi, kwani hutegemea ukubwa wa chembechembe za chokaa kilimo/jasi.

Chembechembe ndogo sana (kwenye hali ya unga unga) ndio ina uwezo mkubwa wa kuyeyuka haraka katika ardhi ikilinganishwa na chembechembe kubwa (punje). Kuyeyuka kwa haraka kwa chokaa kilimo/jasi ndio kunaharakisha kurekebisha pH kwenye udongo.

Ramani ya Tanzania ya afya ya udongo iliyotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) inaonyesha sehemu kubwa ya udongo katika ardhi inayofaa kwa kilimo (arable land) ina viwango tofauti vya pH ya udongo vinavyotakiwa kurekebishwa.

Hivyo wakulima wanatakiwa kutumia chokaa kilimo au jasi kwenye mashamba yao ili kuendana na mahitaji ya udongo.

Changamoto ya matumizi ya chokaa kilimo, jasi

Matumizi ya chokaa kilimo na jasi nchini bado yapo chini ikilinganishwa na kiwango cha udongo ulioathirika kwa tindikali au magad. Changamoto kubwa inayosababisha matumizi ya chokaa kilimo na jasi kuwa madogo ni uelewa mdogo wa wakulima kuhusu umuhimu na matumizi ya chokaa kilimo na jasi.

Pili, uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa kujua afya ya udongo ambapo wakulima wengi wanaendesha shughuli za kilimo kwa mazoea - kulima bila kujua afya ya udongo, hali inayosababisha ama kutumia mbolea nyingi au kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya udongo.

Upatikanaji wa chokaa kilimo, jasi

Viwanda vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) ambavyo vinazalisha chokaa kilimo na Jasi (visaidizi vya mbolea) ni ABM Equipment Services Limited na HSSL Company Limited vyote vya Tanga na Dodoma Cement Company Limited cha Dodoma.

Aina za visaidizi vya mbolea vinavyozalishwa na viwanda hivyo ni kama ifuatavyo:- ABM Equipment Services Limited kinazalisha aina tatu ya visaidizi vya mbolea -- Agricultural gypsum (calcium sulphate), Agricultural Lime (calcium carbonate) na Dolomitic lime (calcium magnesium carbonate); kiwanda cha Dodoma Cement & Company Ltd kinazalisha aina mbili ya visaidizi vya mbolea ambavyo ni Agricultural Lime (Calcium Carbonate) na Agricultural Gypsum (Calcium Sulphate), wakati kiwanda cha HSSL Company Limited kinazalisha aina moja ya chokaa kilimo ambayo ni Agricultural Lime (Calcium Carbonate).

Kwa kuhitimisha, iwapo matumizi ya chokaa kilimo na jasi yatazingatiwa, ufanisi wa mbolea utaongezeka na hivyo kuchochea uzalishaji wa mazao mbalimbali kwa kiwango kikubwa.

• Mwandishi wa makala hii ni Afisa Udhibiti Ubora TFRA

Habari katika Picha

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo akizungumza jambo wakati wa hafla ya jaribio la mbolea itakayozalishwa na kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited kinachojengwa Jijini Dodoma.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Dkt. Godfrey Mkamilo (aliyenyoosha mkono) akieleza matokeo ya jaribio la mbolea aina ya fomi pandia na fomi kuzia baada ya kuitumia katika mashamba darasa wilayani Kilosa. Dkt. Mkamilo alitoa maelezo hayo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Hemed Mwanga, mwezi Mei mwaka huu.

Umati wa wananchi wa Kata ya Kitere waliohudhuria maadhimisho ya siku ya mkulima iliyofanyika Aprili 13, 2022 Mkoani Mtwara.

Habari katika Picha

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara Dunstan Kyobya (aliyefunga mikono katikati) akipongeza timu iliyohusika na uhamasishaji wa matumizi ya mbolea kwa wakulima wa Mikoa ya kusini ikiongozwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa , Wilaya na Mkoa wa Mtwara.

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania na Menejimenti ya Mamlaka wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kumaliza kikao cha bodi kilichofanyika katika Ukumbi uliopo hoteli ya Morena Jijini Dodoma mwishoni mwa mwezi Machi, 2022. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Anthony Mshandete

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Dkt. Godfrey Mkamilo (wa kwanza kulia) akieleza matokeo ya jaribio la mbolea aina ya fomi pandia na fomi kuzia baada ya kuitumia katika mashamba darasa wilayani Kilosa. Wa kwanza kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga.

Wanufaika wa mafunzo ya Sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia tasnia ya mbolea wakionesha vyeti vyao mara baada ya kuhitimu mafunzo hayo.

Wafanyabiashara 135 wa mbolea Kanda ya Ziwa wanolewa

Certificate No.TFRA/AGRO/2021/7369

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF AGRICULTURE
TANZANIA FERTILIZER REGULATORY AUTHORITY

Certificate of Attendance

This is to certify that

ANTHON J. CHARLES

Has Attended the Training Course on Fertilizer Legal Frameworks, Fertilizer Handling and its Judicious Use
At NYAMAGANA DC CONFERENCE HALL- GEITA REGION on 11th-12th MAY, 2022

Gerod Nganilevanu
Ag. Director Regulatory Services

Dr. Stephan E. Ngailo
Executive Director

Moja ya cheti kilichotolewa na Uongozi wa Mamlaka kwa wafanyabiashara wa mbolea waliopewa mafunzo mkoani Mwanza

Na **MWANDISHI WETU**

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Ziwa imefanya mafunzo kwa wafanyabiashara 135 wa mbolea katika halmashauri mbalimbali za kanda hiyo.

Akizungumza na Jarida la ***Mbolea Yetu*** hivi karibuni Kaimu Meneja wa Kanda hiyo Bw. Khanafi Mohamed amesema kuwa mafunzo hayo yalifanyika kwa awamu ambapo mwezi Mei 12 na 13, 2022 yalitolewa katika Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza.

Amesema katika awamu ya pili tarehe 19 na 20 TFRA ilitoa mafunzo katika Wilaya ya Musoma mkoani Mara na kunufaisha wafanyabiashara 42 wa mbolea wakati tarehe 26 hadi 27 Mei, 2022,mafunzo yalitolewa mjini Bariadi mkoani Simiyu ambapo wafanyabiashara 37 wa mkoa huo walinufaika.

Bw. Mohamed amesema mafunzo hayo yalilenga katika kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa mbolea na kuhakikisha wanakidhi matakwa ya sheria ya mbolea na kuhakikisha kuwa wakulima wanapata mbolea zenye ubora.

Bw. Mohamed amesema mada zilizotolewa kwenye mafunzo hayo zililenga maeneo ya sheria ya mbolea, usajili wa mbolea na maombi ya leseni kwa kutumia mfumo wa kimtandao wa Taarifa za Mbolea (FIS), aina za mbolea na virutubisho vya mimea na sifa za maghala ya mbolea.

Mada zingine zilizofundishwa ni kanuni za utunzaji wa mbolea, matumizi sahihi ya mbolea na faida zake, athari za matumizi yasiyo sahihi ya mbolea na utunzaji wa kumbukumbu za biashara ya mbolea.

Aidha, baada ya mafunzo hayo, wadau wa mbolea walitunukiwa vyeti vyenye picha zao ili kuweza kuwabaini pindi ukaguzi wa mbolea unapofanyika katika maeneo yao ya kazi.

Mwaka mmoja wa Rais Samia: Tasnia ya mbolea yazidi kuimarika

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan

Na **MWANDISHI WETU**

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Mhe Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tasnia ya mbolea imeendelea kuimarika na kupata mafanikio katika maeneo mbalimbali chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ni moja ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo yenye jukumu la kusimamia ubora na biashara ya mbolea nchini. Mamlaka imeanzishwa kwa Sheria ya Mbolea Na. 9 ya Mwaka 2009 (Fertilizer Act No 9, 2009) na Kanuni zake za mwaka 2011 na kuanza kutekeleza majukumu yake mnamo Agosti, 2012.

Katika kutekeleza majukumu yake ya udhibiti, Mamlaka inahakikisha kuwa mbolea bora yenye viwango vilivyowekwa kisheria inawafikia wakulima kwa wakati.

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuhamasisha uchumi wa viwanda na kuimarisha mawasiliano na mahusiano na nchi jirani na za ughaibuni kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzitembelea na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini zinazogusa tasnia ya mbolea

Katika kipindi cha mwaka mmoja; Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuhamasisha uchumi wa viwanda na kuimarisha mawasiliano na mahusiano na nchi jirani na za ughaibuni kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzitembelea na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini zinazogusa tasnia ya mbolea.

Miongoni mwa nchi alizotembelea Rais wa awamu ya sita ni pamoja na Burundi, Rwanda, Uganda, Msumbiji, Ufaransa na Ubeligiji. Katika ziara hizo Mhe Rais alitangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini ambapo tasnia ya Mbolea imepata mwekezaji wa kiwanda cha mbolea cha Itracom kutoka nchini Burundi ambapo ujenzi wake unaendelea Jijini Dodoma na uzalishaji unatarajiwa kuanza msimu ujao wa kilimo.

Kuongezeka kwa uwekezaji katika tasnia ya mbolea

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Mhe. Samia, Tanzania imeshuhudia ongezeko la wawekezaji katika tasnia ya mbolea. Ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha ITRACOM jijini Dodoma ni matokeo ya juhudi za serikali ya Awamu ya Sita ambayo imejipambanua kwa kujenga mazingira mazuri na kuvutia wawekezaji ndani na nje ya nchi. Kiwanda hiki kikikamilika kinatarajia kuzalisha tani 600,000 za mbolea na tani 300,000 za mbolea chokaa kwa mwaka kwa kutumia malighafi ambazo kwa sehemu kubwa zitapatikana hapa hapa nchini.

Kufunguliwa kwa kiwanda cha ITRACOM jijini Dodoma ni matokeo ya ziara ya Rais Samia nchini Burundi ikiwa ni miongoni mwa mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita yatakayowezesha kutatua changamoto ya upatikanaji wa mbolea kwa wakulima. Aidha, kitasaidia kuwapunguzia wakulima gharama ya mbolea. Maelekezo ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa kwa kiwanda hicho ni kuhakikisha kuwa uzalishaji unaanza katika msimu wa 2022/2023 ili kutatua changamoto ya bei kubwa za mbolea zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Ujenzi wa kiwanda hiki pamoja na kiwanda cha Minjingu kilichopo mkoani Manyara kutachangia kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea nchini. Kiwanda cha Minjingu kinatarajia kuongeza uzalishaji wa mbolea kutoka tani 100,000 kwa sasa hadi kufikia tani 300,000 mwaka 2023.

Ujenzi wa Maabara ya Mbolea

Serikali awamu ya sita kupitia TFRA inaendelea na ujenzi wa Maabara ya Kimataifa ya Mbolea katika eneo la Kilimo III Vertenary, Temeke, jijini Dar Es Salaam. Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo anaeleza kuwa, ujenzi wa maabara hiyo unasimamiwa na Chuo cha Ufundi Arusha (Arusha Technical College - ATC) kama Mshauri Mwelekezi na unafanyika kwa njia ya "force account" utakaokamilika ifikapo mwezi Julai 2022. Ujenzi huo utakapokamilika unakadiriwa kugharimu takriban kiasi cha shilingi bilioni moja.

>>> *Inaendelea Uk. 18*

Mwaka mmoja wa Rais Samia: Tasnia ya mbolea yazidi kuimarika

Dkt. Ngailo anasema uwepo wa maabara hiyo utasaidia katika kuharakisha upatikanaji wamajibu ya uchambuzi wa sampuli za mbolea na mbolea zinazokidhi viwango vinavyoruhusiwa kuingia sokoni kwa wakati.

Kuimarishwa kwa ofisi za kanda

Kuanzishwa kwa ofisi za kanda ya Kaskazini (Arusha), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Ziwa (Mwanza), Kati (Tabora) kumeiwezesha Mamlaka kutoa huduma kwa wakati katika maeneo waliko wadau bila kuhitajika kufuata huduma hizo makao makuu au watendaji kutoka makao makuu kwenda kutoa huduma katika maeneo hayo. Hii imepunguza gharama na muda kwa upande wa Mamlaka pamoja na wadau. Kutokana na kufungua ofisi za kanda, mamlaka katika kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Disemba, 2021), Mamlaka kupitia makao makuu na ofisi zake za kanda, imefanya mafunzo kwa wafanyabiashara wa mbolea 2,483 kutoka katika mikoa ya Songwe (182), Rukwa (46), Katavi (40), Mbeya (228), Ruvuma (222), Njombe (262), Iringa (169), Arusha (77), Kilimanjaro (78), Tanga (60), Manyara (26), Mtwara (160), Lindi (175) na Morogoro (758). Idadi ya wafanyabiashara waliopatiwa mafunzo katika kipindi cha nusu mwaka ni asilimia 98 ya idadi ya wafanyabiashara 2,521 waliopatiwa mafunzo mwaka jana (2020/21). Mafanikio hayo ni kutokana na Mamlaka kuongeza nguvu kazi na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu kati ya watumishi wa kanda na makao makuu.

Kutoa huduma kwa wateja kwa njia ya kielektroniki

Serikali ya Awamu ya Sita, imeiwezesha Mamlaka kuimarisha utoaji huduma kwa kuanzisha Mfumo wa Kimtandao wa Mbolea (Fertilizer Information System - FIS) ambao umeboresha utoaji wa huduma kwa wateja, kwa kutoa huduma za usajili wa wafanyabiashara wa mbolea na utoaji wa leseni, vibali vya kutoa na kuingiza mbolea nchini na usajili wa mbolea. Tangu kuanza kutumika kwake mwezi Machi 2021, mfumo umeongeza ufanisi na kupunguza adha ya utoaji na upatikanaji wa huduma zinazotolewa na Mamlaka.

Meneja wa TEHAMA na Takwimu Robert Mtendamema anasema mfumo wa FIS umekuwa ukombozi kwa wadau wa mbolea nchini kwani kwa sasa wanapata huduma kwa haraka ikilinganisha na kabla ya kuwepo kwa mfumo huo. "Upatikanaji wa leseni za wafanyabiashara wa mbolea kwa kutumia mfumo unachukua chini ya masaa 24 ukilinganisha na siku 3 hadi 7 kabla ya mfumo" anasema Mtendamema.

Viwanda vya ndani vya mbolea vyaongezeka

Pamoja na kuwepo kwa mwekezaji mkubwa wa mbolea Jijini Dodoma, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolela Tanzania (TFRA) imeendelea kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa mbolea kwa kutoa elimu pamoja na kuwaonesha njia wazalishaji wadogo ya kutatua changamoto za mitaji kwa kuwakutanisha na taasisi za kifedha na wakala wanaotoa huduma za mikopo ya vifaa kwa wajasiriamali wadogo nchini.

Hivi karibuni wataalam kutoka TFRA walipiga kambi Jijini Arusha na kutoa mafunzo kwa wazalishaji wadogo wa Mbolea wa Kanda ya Kaskazini ambapo wazalishaji hao walikutanishwa na wataalam kutoka Shirika (SIDO), EFTA, PASS, CRDB bank na NMB banki ili kuwajengea uwezo wa namna ya kuimarisha uwekezaji wao pamoja na kupata ushauri wa kitaalamu katika masuala ya kimitaji.

Akizungumza katika kikao kazi hicho, Kaimu Meneja wa Uzalishaji wa Ndani na Mazingira, Stephenson Ngoda anasema, kwa sasa kuongeza uzalishaji wa ndani wa mbolea ndiyo ajenda ya kitaifa. Anatumia fursa hiyo kuwahamasisha wazalishaji wadogo kuongeza uzalishaji wa mbolea yenye viwango vinavyokubalika itakayotosheleza mahitaji ya nchi na kubainisha rasilimali kwa ajili ya uzalishaji huo zinapatikana nchini.

> **Serikali ya Awamu ya Sita** imeiwezesha Mamlaka kuimarisha utoaji huduma kwa kuanzisha Mfumo wa Kimtandao wa Mbolea ambao umeboresha utoaji wa huduma kwa wateja, kwa kutoa huduma za usajili wa wafanyabiashara wa mbolea, utoaji wa leseni, vibali vya kutoa na kuingiza mbolea nchini pamoja na usajili wa mbolea

Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini

Kwa mwaka 2020/2021 matumizi ya mbolea nchini yaliongezeka na kuwa tani 475,870 huku upatikanaji ukiwa ni tani 766,024. Ongezeko la matumizi ya mbolea linatokana na kuwepo kwa sera wezeshi za uingizaji na usambazaji wa mbolea nchini.

Aidha, elimu imekuwa ikitolewa mara kwa mara juu ya umuhimu wa matumizi bora ya mbolea kwa kilimo endelevu na chenye tija. Upatikanaji wa mbolea umeongezeka kwa kuweka mazingira wezeshi ya biashara ya mbolea na usafirishaji wa mbolea nje ya nchi kwa lengo la kuongeza mapato ya nchi kupitia mbolea zinazopita nchini kwenda nchi jirani.

Tanzania imeendelea kuwa miongoni mwa nchi barani Afrika inayoendelea kuongeza matumizi ya mbolea mwaka kwa mwaka kufikia maazimio ya Azimio la Maputo (The Maputo Declaration 2003) la kuongeza matumizi ya mbolea katika eneo la ukanda wa nchi zilizo chini ya jangwa la Sahara (SADC) la kufikia angalau kilo 50 za viinilishe kwa hekta.

Udhibiti wa mbolea

Akizungumzia mafanikio katika suala la udhibiti wa mbolea katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti Gerod Nganilevanu anasema katika kipindi cha mwaka 2020/21 na mwaka 2021/2022 jumla ya wafanyabiashara 2,521 wamepewa mafunzo juu ya utunzaji na uhifadhi wa mbolea kutoka katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Tanga, Singida, Dodoma, Tabora, Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga, Geita, Kagera, Ruvuma, Njombe, Iringa, Katavi, Rukwa, Mbeya, na Songwe, vilevile wanafunzi 293 kutoka chuo cha kilimo MATI – Ukiriguru nao walipewa mafunzo hayo.

Anasema, idadi hiyo ni ongezeko la asilimia 64.4 ya idadi ya wafanyabiashara 1,534 waliopatiwa mafunzo mwaka 2019/2020.

Kufuatia ukweli kuwa sekta ya kilimo ni sekta inayobeba watanzania wengi serikali inapongezwa kwa kuweka nguvu kubwa ya kutaka kuwainua wakulima ili kuweza kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na hivyo kuongeza pato la mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Orodha ya Mbolea na Visaidizi vya Mbolea vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Mbolea, 2009

Na	Namba ya Usajili	Jina la Biashara la Mbolea	Kiwango cha Virutubisho	Mwaka wa Usajili
1	0001	Urea	46%N	2012
2	0002	Di-Ammonium Phosphate (DAP)	18%N: 46%P2O5	2012
3	0003	Mono Ammonium Phosphate (MAP)	11-12%N: 48-61%P2O5	2016
4	0004	Calcium Ammonium Nitrate (CAN)	26-27%N	2012
5	0005	Ammonium Sulphate (SA)	21%N + 24% S	2012
6	0006	Triple Super Phosphate (TSP)	46%P2O5	2012
7	0007	Potassium Chloride (Muriate of Potash (MOP)	60%K2O	2012
8	0008	NPK 25:5:5	25%N: 5%P2O5: 5%K2O	2012
9	0009	NPK 17:17:17	17%N: 17%P2O5: 17%K2O	2012
10	0010	NPK 16:16:16	16%N: 16%P2O5: 16%K2O	2012
11	0011	NPK 20:10:10	20%N: 10%P2O5: 10%K2O	2012
12	0012	NPK 10:18:24	10%N: 18%P2O5: 24%K2O	2012
13	0013	Sulphate of Potash (SOP)	48-53%K2O + 17-18%S	2015
14	0014	NPK	6%N: 24%P2O5: 20%K2O + 1.5%Mg, 8%S, 0.25%B, Zn	2012
15	0015	NPK	5%N: 20%P2O5: 24%K2O + 1%Mg, 10%S, 0.25%B, Zn	2012
21	0021	Coating Material (Avail, Nutris)	1.5%Zn, 0.5%Mn	2012
22	0022	Minjingu Nafaka plus	9%N: 18%P2O5: 6%K2O + 25%CaO, 2%MgO, 5%S,0.1%B,0.5%Zn	2018
23	0023	Magnesium Nitrate	11%N +15%MgO	2012
24	0024	NPK 23:10:5	23%N: 10%P205: 5%K20	2012
25	0025	Plant Catalyst	0.00002728% Cacl2, 0.00002728% MgSO4, 0.000798% Sulfate Castor Oil, 0.00596% Sodium Metasilicate, 1% Lignite Extract	2020
26	0026	NPK 23:21:0 + 4 S	23%N: 21%P2O5: 0%K2O + 4%S	2012
27	0027	NPK 22:6:12	22%N: 6%P2O5: 12%K2O + 2%CaO, 3%S, 1%MgO, 0.2%B, 0.2%Zn	2012
28	0028	Calcium Nitrate	15.5%N + 26.5%CaO	2015
30	0030	Poly NPK 17:17:17	17%N: 17%P2O5: 17%K2O	2016
31	0031	NPK 15:9:20+TE	15%N: 9%P2O5: 20%K2O + TE	2018
32	0032	S Poly NPK 8:14:19	8%N: 14%P2O5: 19%K2O	2016
33	0033	Poly NPK 8:14:19	8%N: 14%P2O5: 19%K2O	2016
34	0034	Booster IIC	32%N: 10%P2O5: 8K2O + TE	2016
35	0035	NPK 15:15:15	15%N: 15%P2O5: 15%K2O	2016
36	0036	Maxi MKP	52%P2O5: 34%K2O	2016
38	0038	Maxi KS	50%K2O + 3%H2SO4	2016
39	0039	Max Magna N	15% MgO + 98% Mg (NO3)2	2016
40	0043	Tecamin Raiz	5.5%N: 0% P205: 1%K2O + 0.05%B, 0.15%Zn, 0.5%Fe, 0.05%Cu, 0.3%Mn,4.7% Amino Acids, 22%OM	2016
41	0044	Agro Feed Plus	12%N: 10% P2O5: 8%K2O + TE	2013

42	0045	MAXI Map	61.5%P2O5 + 12.1% NH4	2016
43	0050	Micro Nutrients (Zinc Sulphate Heptahydrate)	0.3%Mg,11%S, 21.5%Zn, 0.004%Cu	2013
44	0053	Easy grow starter	18%N: 20%P2O5: 21%K2O	2013
45	0054	Pot Phos	0%N: 50%P2O5: 30%K2O	2016
46	0055	NPK 14:0:2 + 13Ca + 2.5Mg	14%N: 0% P2O5: 0.2%K2O + 13%CaO, 2.5%Mg + TE	2013
50	0056	Agriculture Lime (Calcium Carbon-ate)	CaCO3	2015
53	0057	Agriculture Gypsum (Calcium Sulphate)	CaSO4.2H20	*2015*
54	0058	Easy grow Flower and Fruits	14%N: 11%P2O5: 33%K2O	2013
55	0059	Easy gro Vegetative	27%N: 10%P2O5: 16%K2O	2013
56	0060	MAXI Magna S	16%MgO + 12.5% S	2016
57	0061	MAXI Calci N	15.5% N + 18.5% Ca	2016
58	0062	MAXI K	13%N: 46% K2O	2016
59	0063	Potassium Nitrate	13%N: 44%K2O	2012
60	0064	Nutrivant Plus Malt Barley	23%P2O5: 42%K2O + 0.1%B, 0.5%Zn, FV	2013
61	0065	Nutrivant Plus Potato	43%P2O5: 28%K2O + 2%MgO, 0.5%B, 0.2%Mn	2013
62	0066	Max More	15%N: 15%P2O5: 15%K2O	2016
63	0067	Novacid	19%N: 19%P2O5: 19%K2O + 3%MgO + Me	2013
64	0068	Nutrivant Plus Rice	46%P2O5: 30%K2O + 2%MgO, 0.2%B, FV	2013
65	0069	Novacid	11%N: 7%P2O5: 28%K2O + 2%MgO + Me	2013
66	0070	Novacid	12%N: 8%P2O5: 23%K20 + 2%MgO + Me	2013
67	0071	Novacid	16%N: 8%P2O5: 16%K2O + 8%MgO + Me	2013
68	0072	Nova N:P:K + TE	20%N: 9%P2O5: 20%K2O + TE	2013
69	0073	Nova N:P:K	19%N: 19%P2O5: 19%K2O + MgO + TE	2013
70	0074	Nutrivant	18%N: 24%P2O5: 18%K2O + TE	2013
71	0076	Fe Eddha (Micro Nutrients)	6% Fe	2016
72	0078	Minjingu Mazao NPS	10%N: 20%P2O5 + 25%CaO, 5%S, 0.5%Zn	2015
73	0079	Yaraliva Nitrabor	15.4%N + 25.6%CaO, 0.3% B	2018
74	0080	Yaravera Amidas	40%N + 5.5%S	2018
76	0081	NPK 14:14:20 + MgO + 0.1 B	14%N: 14%P2O5: 20%K2O + MgO, 0.1% B	2013
78	0082	Yaramila Winner	15%N: 9%P2O5: 20%K2O + 3.8%S, 1.8%Mg, 0.02%B, 0.02%Mn, 0.02%Zn	2018
79	0083	Yarabela Sulfan	24%N + 10.7%CaO, 6%S	2018
80	0084	Agroblen	20%N: 10%P2O5: 10%K2O + 4Mg	2013
81	0085	Poly-Booster	21%N: 21%P2O5: 21%K2O	2016
82	0087	Potassium Nitrate	13% N, 44% K2O, 0.5% CaO, 0.5% MgO	2016
83	0088	Magnesium Sulphate	99% MgSO4	2016
84	0089	NPK 13:2:44	13%N: 2% P2O5:44% K2O	2016
85	0090	Nutrivant Plus	19%N: 19%P2O5: 19%K2O + 2%MgO + B + Me	2015
87	0091	Ammoniated Concentrated Super-	4-6% N: 19-21% P_2O_5	
88	0092	Kyto Booster	12%N: 10%P_2O_5: 8%K2O	2021
89	0095	NPK 10:10:24	10%N: 10%P2O5: 24%K20	2014
90	0096	Sumicoat303	15% N: 36% P2O5: 0% K20	2018
91	0097	Nutrivant NPK	31%N: 0%P2O5: 7K2O + 2% MgO + TE + FV	2016
92	0098	Nutrivant NPK	6%N: 18%P2O5: 37% K2O5 +2% MgO + TE + FV	2016

95	0099	Fertigrain Foliar	5%N + 0.1%B, 0.75%Zn, 0.1%Fe, 0.1%Cu 0.5%Mn, 0.02%Mo, 0.01%Co, 40%OM, 10% Amino Acids	2016
96		Tecamin Max	7%N + 14.4% Amino Acids	2016
97		Tecamin Flower	3% N: 10% P2O5 + 1%B, 0.5%Mo, 3% Amino Acids	2016
98	0102	NPK 22:6:12	22%N: 6%P2O5: 12%K2O	2014
99	0103	Agriful	4.5% N: 1% P2O5: 1%K2O + 25% Fluvic Acids, 25%Humic Extract, 45%OM	2016
100	0104	NPK 4:3:3 FERTIPLUS	4%N: 3%P2O5: 3%K2O	2016
101	0105	NPK	10%N: 18%P2O5: 24%K2O + 7S	2016
102	0106	Maxi Force Fruiter	5%N: 5%P2O5: 40%K2O + 0.25%MgO + TE	2020
103	0107	Murphy Foliar Feed	22%N: 21%P2O5: 17%K 2O	2020
104	0108	Omex foliar	24%N: 24%P2O5: 18%K2O + TE	2014
105	0110	YaraVita Power Boost	4.8%N + 4.9%Mg + 4.9%B + 9.9%Zn	2020
106	0111	YaraVita Crop Boost	0%N: 30%P2O5: 5%K2O + 2.5%Mg + 3.1%Zn	2020
107	0112	Biofix	Biofix-Legume Inoculant	2016
108	0113	Rokohumin Loose	7% + 49% Humic acid	2020
110	0114	Agrigrow Starter	14%N: 28%P2O5: 18%K2O + TE	2017
111	0115	Multigro	19%N: 19%P2O5: 19%K2O + TE	2017
112	0116	Fastgro	12%N: 10%P2O5: 8%K2O + TE	2017
113	0117	Hakika	1.5%N: 1.5%P2O5: 3.5%K2O + 25% Organic Matter	2020
114	0118	Legumefix	Rhizobia Bacteria	2015
115	0119	Max More fertilizer	10%N: 5%P2O5: 40%K2O + TE	2016
116	0120	NPK	25%N: 5%P2O5: 5%K2O + 5%S	2016
117	0121	Soil Plus (Compost)	2.1%N: 3.6%K2O	2020
118	0122	Booster Sic	16%N: 10%P2O5: 8%K2O	2020
119	0123	Booster Sic	16%N:	
120	0124	Urea Coated Sulfur	40%N + 7%S	2016
121	0125	Granubor Natur	15% B	2015
122	0126	Sulfur coated CAN	24%N + 15%S	2015
123	0127	Activit	4%N: 3%P2O5: 2%K2O	2016
124	0128	Sulphate of Potash	51%K20 + 18%S +1%Cl	2015
125	0129	Zinc 700	70%Zn	2016
126	0130	Bontera	Bacillus, Rhizobium	2016
127	0131	Boron 15	15%B	2016
128	0132	Nutrivant High K	6%N: 18%P2O5: 37%K2O + 2%MgO, ME, FV	2021
129	0133	NPK 17:21:11	17%N: 21%P2O5: 11%K2O	2016
130	0134	Seaweed Liquid Organic Fertilizer	13.44% N: 7.55% P2O5: 4.84%K2O	2021
131	0135	Green Sea	0.6%Mg, 0.2%B, 0.4%Zn, 0.2%Fe, 0.9%Cu	2017
132	0136	Dodoma Aglime	97.56% Calcium Carbonate	2016
133	0137	Multi K	13%N: 46%K2O	2016
134	0138	Nutrivant High P	8%N: 50%P2O5: 8%K2O + 2 %MgO, ME, FV	2021
135	0139	Nutrivant High N	31%N: 8%P2O5: 7%K2O + 2 %MgO, B, ME	2021
136	0140	Nutrivant Balance	19%N: 19%P2O5: 19%K2O + 2%MgO, ME, FV	2021
137	0141	Calcium Magnesium Carbonate (Dolomite Lime)	48% CaCO3, 38% MgCO3, 67% ECCE	2021
138	0142	Afro Total	20%N: 20%P2O5: 20%K2O	2021
139	0143	Afro Kuza	30%N: 10%P2O5: 10%K2O	2021
140	0144	Afro Finisher	10%N: 10%P2O5: 40%K2O	2021

141	0145	Afro Starter	10%N: 52%P2O5: 10%K2O	2021
142	0146	Wuxual Macromix	24%N: 24%P2O5: 18%K2O	2016
143	0147	Polyfeed	26%N: 8%P2O5: 17%K2O + 2%MgO	2016
144	0148	Polycoffee	19%N: 19%P2O5: 19%K2O	2016
145	0149	Mono Potassium Phosphate	0%N: 51.5%P2O5: 34%K20	2016
146	0150	NPK	8%N: 24%P2O5: 16%K2O + 5%S, 0.1%B, 0.5%Zn	2016
147	0151	Minjingu Organic Hyperphos-phate (Powder)	28%P2O5 + 36%CaO	2013
148	0152	Minjingu Organic Hyperphos-phate (Granular)	28%P2O5 + 36%CaO	2013
149	0153	Mokusaku Cal - Phos	O%N: 0.7%P2O5: 0.5%K2O + 5%Ca, 0.5% Mg	2021
150	0154	Mafanikio Farm Booster	32% N: 10%P2O5: 8%K2O	2021
151	0155	Polihalite	14%K2O + 17%CaO, 6%MgO, 47.8%SO3	2016
152	0156	Synthentic polyhalite	14%K2O + 17%CaO, 6%MgO, 47.8%SO3	2016
153	0157	Poly NPK 20:10:10	20%N: 10%P2O5: 10%K2O	2016
154	0158	S Poly NPK 20:10:10	20%N: 10%P2O5: 10%K2O	2016
155	0159	S Poly NPK 17:17:17	17%N: 17%P2O5: 17%K2O	2016
156	0160	Bioflush	49.3% Protein + 3.1 Soluble Carbohydrate	2018
157	0161	Yad Bio Vitalizer	2.45%N: 0.76%P2O5: 2.66%K2O + 13%CaO, 1.01%B	2018
158	0162	Positive booster plus	12%N: 10%P2O5: 8%K2O + TE	2018
159	0163	Falmax O.P. F	2%N: 10%P2O5: 01%K2O + TE	2018
160	0164	Kristal (Magnesium Sulphate)	16%Mg + 13%S	2018
161	0165	Mazao Super Fruit & Flower	15%N: 10%P2O5: 35%K2O + TE	2018
162	0166	Yara rega	20%N: 5%P2O5: 18%K2O + Zn, B	2018
163	0167	Osmocote	18%N: 6%P2O5: 12%K2O	2018
164	0168	Boom flower	11%N: 8%P2O5: 6%K2O +TE	2016
165	0169	Snow fert	19%N: 19%P2O5: 19%K2O+ TE	2018
166	0170	Kynoplus	46 % N + 5% Zn	2018
167	0171	Sugar Oemff	9%N: 5%P2O5: 8%K2O	2016
168	0172	Green Gold	33% N	2018
169	0173	Kynopop	14%N: 09%P205: 04%K2O	2018
170	0174	Vitalon 2000	7.3% Titanic Sulphate, 1.2% Citric acid, 0.3% Tartaric acid, 4.2% Ammonia water, 1% Acticide	2021
171	0175	Mo-quick	20%N: 20%P2O5: 20%K2O	2018
172	0176	Vita booster plus	15%N: 10%P2O5: 34%K2O + TE	2018
173	0177	YaraMila Cereal	23%N: 10%P2O5: 05%K2O + 2%MgO +3%S + 0.3%Zn	2018
174	0178	Mazao Super (Total)	20%N: 20%P2O5: 20%K2O + TE	2018
175	0179	Mazao Super (Vegetative)	28%N: 14%P2O5: 14%K2O + TE	2018
176	0180	NPK	14%N: 23%P2O5: 14%K2O + 5%S +1% B2O3	2018
177	0181	Boom flower	2.2% Aromatic Nitrogen	2018
178	0182	Foliar Booster Potato NPK 14:2	14%N: 25%P2O5: 13%K2O + TE	2018
179	0183	Foliar Booster High P, NPK 13:	13%N: 52%P2O5: 05%K2O + TE	2018
180	0184	Crop Master NPK 24:18:18	24%N: 18%P2O5: 18%K2O + TE	2018
181	0185	Foliar Booster High N NPK 31:1	31%N: 11%P2O5: 11%K2O + TE	2018
182	0186	Foliar Booster high K NPK 15:1	15%N: 12%P2O5: 31%K2O	2018
183	0187	NPS	19%N: 38%P2O5: 0%K2O + 7%S	2018
184	0188	SumiCoat 60	13%N: 10%P2O5: 13%K2O	2018

185	0189	Synergizer	8%N: 32% P2O5: 4%K2O	2018
186	0190	Gro plus	O%N: 50%P2O5: 35%K2O	2018
187	0174	Polyfeed	28%N: 14% P2O5: 14%K2O	2017
188	0192	Fast grow fruit & Flower	14%N: 11%P2O5: 33%K2O + TE	2018
189	0193	Fast grow vetetative	27%N: 10%P2O5: 16%K2O +TE	2018
190	0194	Black alg	2%K2O + Organic Nutrients	2018
191	0195	Almina	1%N: O%P2O5 :2%K2O + Organic Nutrients	2018
192	0196	Agromaster	24%N: 6%P2O5: 12%K2O	2017
193	0197	Poly Sulphate	11.6%K2O + 12.1%CaO, 3.6%Mg, 19.2% S	2017
194	0198	Nov Acid	16%N: 32%P2O5: 16%K2O	2017
195	0199	Novacid	16%N: 8%P2O5: 25%K2O	2017
196	0200	Omex Foliar Feed	24%N: 24%P205: 18%K20 + TE	2017
197	0201	Omex Murex K	Bacterial and Algae Extract	2017
198	0202	Omex CalMax	15%N: 22.5%CaO	2017
199	0203	Biopower (Grow Power)	Bacterial and Algae Extract	2017
200	0204	BioForce	Etract of See Weed and Blue Green Algae	2017
201	0205	Berrylon	Etract of See Weed and Blue Green Algae	2017
202	0206	Biopower Plus	30% Sea Weed Extract, 4g/L Cu + Zn + Mo + B, 12%N: 20%P2O5: 20%K2O	2017
203	0207	Wuxal Super Amino	8%N: 8%P2O5: 6%K2O	2017
204	0208	Wuxal Microplant	5%N: 10%P2O5: 3%K2O + 1%Zn 1%Fe, 1.5%Mn,	2017
205	0209	Amcolon Suspension	24%N: 24%P2O5: 18%K2O + 1.5%Mg	2017
206	0210	Amcopaste	20%N: 20%P2O5: 20%K2O	2017
207	0211	Amcopaste	5%N: 50%P2O5: 30%K2O	2017
208	0212	Amcolon	20%N: 20%P2O5: 20%K2O +TE	2017
209	0213	Mofcal	12%N + 5%Mg, 15% CaO	2017
210	0214	Amcopotato	14%N: 25%P2O5: 13%K2O + 3.2%Mg, 12.5%S, 1.8% Zn	2017
211	0215	Amcofert	O%N: 30%P205: 40%K2O + TE	2017
212	0216	Amco KTS	36%K2O + 25% S	2017
213	0217	Goldfert	10%N: 50%P2O5: 10%K2O	2017
214	0218	Mult N	40% N	2017
215	0219	Foliboost	8.5%N + 4%B, 4% Zn, 40%C, 13.5% Amino Acid	2017
216	0220	Amcopaste	18%N: 44%P2O5	2017
217	0221	Amcopaste	15%N: 20%P2O5: 50%K2O	2017
218	0222	Amcolon	10%N: 50%P2O5: 10%K2O	2017
219	0223	Omya Calciprill 110-LF	38%CaO + 0.6%Mg	2017
220	0224	Omya Magprill	25%CaO + 9.5%Mg	2017
221	0225	Bioenzyme	0.1%Mg, 0.4%S, 0.3%B, 0.3%Zn, 0.4%Fe, 0.1%Mn	2017
222	0226	Foltron Plus	5.6%N: 19.5%P2O5: 5%K2O + TE	2017
223	0227	Pilatus	4.9%Zn + 17% Organic Matter	2017
224	0228	YaraMila otesha	12%N: 24%P2O5: 12%K2O + 2%MgO, 5%S, 0.007%Zn 0.2%Fe,	2017
225	0229	Bio - TBB	*Streptomycetes sp, Lactobacillus sp, Actinomycetes, Rhizobium sp, Azotobacter sp, Citrobactor sp*	2017
226	0230	Bio - TRENT	*Streptomycetes sp, Lactobacillus sp, Rhizobium sp*	2017
227	0231	Kilimo Booster Plus	19%N: 19%P2O5: 10%K2O	2017
228	0232	Sulphur Maji	8.5% S	2017

229	0233	Vegimax	1.1%N: 0.13%P2O5: 3.9%K2O +0.58%CaO, 0.48%Mg, 0.38%S, 29.45% Organic Matter	2017
230	0235	PK Fertilizer	51.5%P2O5: 34%K2O	2017
231	0236	Fruit King	0.5%B, 051%Zn, 0.31%(6-BA)	2017
232	0237	Root King	0.62%IBA	2017
233	0238	Cytokinin Moreking	0.4% Cytokinin	2017
235	0239	Nutriplant Organic Plus Fertilizer	0.005%CaO, 0.007%Mg, 1.62%Zn 22%Fe, 0.001% Cu, 0.24%Mn,	2017
236	0240	Tecamin Brix	18%K2O + 0.2% B	2017
237	0241	Tecnokel Amino Cab	10%CaO, 0.2%B, 6% Amino acid	2017
238	0242	Fertigrain Start	3%N + 9% B, 30% OM	2017
239	0243	Agriphyt contact ZnMn	1.5%Zn, 0.5%Mn	2017
240	0244	Controlphyt Cu	6.5%Cu	2017
241	0245	Kanmetal	1%Zn, 0.5%B, 2%Fe, 0.5%Cu, 1%Mn	2017
242	0246	Kankompoze	8%N: 9%P2O5: 13%K2O	2017
243	0247	Kangrow	3%N: 2%K2O	2017
244	0248	Kanpotas	30%P2O5	2017
245	0249	Compound D	30% Humic acid + 10% Ascorbic acid	2017
246	0250	Hai 450	1.4%N: 0.3%P2O5: 0.7%K2O +2.5%OM	2017
247	0251	Alvirus	2.5%Cu	2017
248	0252	D.I Grow	2.35%N: 4.44%P2O5: 1.75%K2O + TE	2017
249	0255	Agri Grow Vegetative	30%N: 10%P2O5: 10%K2O + TE	2017
250	0256	Agrigrow Fruiting& Flowering	15%N: 5%P2O5: 35%K2O + TE	2017
251	0257	Allwin Top	28%N: 8%P2O5: 9%K2O + TE	2017
252	0258	Agrichem Folia	12%N: 10%P2O5: 10%K2O + TE	2017
255	0259	Yara Vita Trace BZ	5%N: 7.5% P2O5: 5%K2O + 5%Mg 5%S, 5%B, 5%Zn, 0.1%Fe, 0.1%Cu, 0.1%Mn, 0.1%Mo	2014
256	0260	Yara Vita Cereal Boot	O%N: 29.5%P2O5: 5%K2O+ 2.7%MgO + 3.1%Zn	2014
257	0261	Yara Vita Zintrac 700	Conc. Zinc micronutrient	2014
258	0262	Yara Vita Bortrac 150	10.9%B	2016
259	0263	Yara vita coptrac dual	33% Cu	2018
260	0264	Mo-wonder	18%N: 6%P205: 9%K20	2018
261	0265	Mo-top	28%N: 8%P2O5: 9%K2O + 4%B	2018
262	0266	Mo-eliixer	11%N: 7%P2O5: 7%K2O	2018
263	0267	Elit N	25%N	2018
264	0268	Truva	5%N: 25%P2O5	2018
265	0269	Safir 21	2%K2O + Organic nutrients	2018
266	0270	Zincop	3%N: 15%P2O5 +10%Zn	2018
267	0271	Exelans	5%N: 0% P2O5: 5%K2O +25%OM + TE	2018
268	0272	Nessmix	0.5%B, 4%Zn,4%Fe, 0.5%Cu 2%Mn	2018
269	0273	Sweet K	30%K2O	2018
270	0274	Erth Food	1.6%N: 0.5%P2O5: 0.5%K2O + 60%OM	2018
271	0275	NPK Zn	11%N: 22%P2O5: 21%K2O +4%S, 1%B +0.1%zn	2018
272	0276	Golden leaf tobacco	10%N: 18%P2O5: 24%K2O + 7%CaO, 0.5%MgO, 7%S,0.1%B	2018
273	0277	Minjingu Top dressing/Caan plus Top dressing	27%N: 10%P2O5: 0%K20 + 15%CaO	2018
274	0278	Mielle oemf	8%N: 17%P2O5: 2%K2O	2018
275	0279	Veggie oemf	08%N: 05%P2O5: 30K2O	2018

276	0280	Oc-booster	31%N: 10%P2O5: 8%K2O + TE	2018
277	0281	Rizoliq Soy	Bradyrhizobium Japonicum	2018
278	0282	Mengi mavuno	20%N: 20%P205: 20%K20 + TE	2018
279	0283	Maxiforce starter	15%N: 30%P2O5:15%K2O + 1% MgO + TE	2018
280	0284	Maxiforce Grower	30%N: 10%P2O5: 10%K2O + 0.7%MgO + TE	2018
281	0285	Maxiforce fruiter	10%N: 10%P2O5: 40%K2O + 1% MgO + TE	2018
282	0286	NPS Zn	12%N: 45%P2O5 + 5% S + 1% Zn	2018
283	0287	G - One	0.05%Fulvic Acid	2019
284	0288	Grow -Cal	10%N + 17%CaO, 14%Mg,0.1%B	2018
285	0289	Paristar	30% Humic acid + 10% Ascorbic acid	2019
286	0290	Verno Fg	30% Zn + 30% Cu	2019
287	0291	RTS 7:7:7	7%N: 7% P2O5: 7% K2O	2019
288	0292	Tanzanite Booster Plus	19.87%N: 11.74%P2O5: 11.11%K2O + 0.001%Zn, 0.04%Fe + 0.009%Cu, 0.026%Mn	2019
289	0293	Mokusaku NPK Plus	3.67%N: 2.25%P2O5: 0.7%K2O + 0.3%Ca, 0.07%Mg	2021
290	0294	Techoel Amino Mn	2.93%N + 6.99%Mn	2019
291	0295	Controlphyt PK	29%P2O5 + 21.6%K2O	2019
292	0296	Technophyt Ph+	3%N + 29%P2O5	2019
293	0297	Technokel Amino B	10%B	2019
294	0298	Soil king slari asilia ya kibiologia	0.02%K2O + 0.01%CaO + 0.06%Na	2019
295	0299	Soil king mbolea halisi	0.06%N: 0.01%P2O5: 0.15%K2O + 0.03%CaO	2019
296	0300	Saprolife	2.5%N: 0.3%P2O5: 0.12%K2O + Te	2019
297	0301	Vitazyme Micro Foliar	0.15%Zn, 0.5%Fe, 0.05%Cu	2020
298	0302	Fastgrow Starter	18%N: 20%P2O5: 21%K2O + TE	2020
299	0303	Fastgrow Foliar Feed	12%N: 12%P2O5: 12%K2O + TE	2020
300	0304	Ferrelene- Fe EDDHA	6%Fe	2020
301	0305	Elfert- F	4.1%MgO ,1.12%B, 2.9%Zn 5.4%Fe, 0.67%Cu, 2.83%Mn, 0.048%Mo	2020
302	0306	Giant	0%N: 45%P2O5: 55%K2O	2020
303	0307	Micronet-15	2%MgO, 1.5%B, 4%Zn, 4%Fe, 0.5%Cu, 3%Mn, 0.05%Mo	2020
304	0308	Suspension 12-12-44	12%N: 12%P2O5: 44%K2O + 3%MgO + TE	2020
305	0309	Suspension 24-24-14	24%N: 24%P2O5: 14%K2O	2020
306	0310	Mazao Booster	32%N: 10%P2O5: 20%K2O + 20%S, 2%B 2%Zn, 2.8%Fe, 3.7%Cu, 2.7%Mn, 2%Mo, 2.8%Co	2020
307	0311	Agromaster	16%N: 10%P2O5: 22%K2O	2020
308	0312	Humic plus	12.17%K2O + 71.07 % Humic acid	2020
309	0313	Neo Supreme	24%N: 24%P2O5: 18%K2O + 4%Mg, 4%S, TE	2020
310	0314	Neo High P	12%N: 45%P2O5: 20%K2O + 2%CaO, 4%Mg, TE	2020
311	0315	Super Neo High K	15%N: 10%P2O5: 45%K2O + 4%Mg, 4%S, TE	2020
312	0316	Micronet -36	12%N +18%CaO, 3%Mg, 1%B, 2% Amin acid	2020
313	0317	Superfeed	19%N: 19%P2O5: 19%K2O + Mg + TE	2020
314	0318	TFA Fahari (Myco Sol)	12%N: 6%K2O + 40%SO3	2021
315	0319	Agromaster	15%N: 24%P2O5: 12%K2O	2020
316	0320	Fahari Booster	20%N: 20%P2O5: 18%K2O + TE	2020
317	0321	Rokohumin-Duplo	5.65%N: 0.9%P2O5: 4.61%K2O	2020
318	0322	Aviel Extra Booster	20%N: 5%P2O5: 35%K2O	2020
319	0323	Potassium Schonite	23%K2O + 11%MgO	2020

320	0324	Max Yield	15%N: 10%P2O5: 45%K2O	2020
321	0325	Max Green	31%N: 11%P2O5: 15%K2O	2020
322	0326	Fast Crop Max-K	15%N: 10%P2O5: 45%K2O + 4%MgO, 4%S,	2020
323	0327	Gap Mbolea	12%N: 12%P2O5: 12%K2O	2020
324	0328	Keenfeeder's Booster	12%N	2020
325	0329	Keen Mavuno	15%N: 15%P2O5: 15%K2O + TE	2020
326	0330	New Victory Booster	19%N: 19%P2O5: 10%K2O	2020
327	0331	Sulotaste	19%N: 19%P2O5: 19%K2O + MgO, TE	2020
328	0332	Organic Fertilizer	2.3% N + 18.6% C/N, 42.8% OC, 38% OM,	2021
329	0333	Groforce	2% N: 0.1% P2O5: 4% K2O + 8 g/l Mg, 20 g/l Amino Acid, 200 g/l Organic Matter, 8 g/l Humic Acid, 120 g/l Organic Sugar	2021
330	0334	BM Start	1.7% N + 2.1% MgO, 2.07% B, 0.02% Mo, 2.84% H2SO3	2021
331	0335	FarmGrow Vegetative	38%N: 5%P2O5: 5%K2O	2021
332	0336	FarmGrow Starter	13%N: 40%P2O5: 13%K2O + TE	2021
333	0337	F100	8%N: 2%P2O5: 8%K2O	2021
334	0338	F300	2%N: 11%P2O5: 11%K2O	2021
335	0339	Full Power	12%N: 18%P2O5: 12%K2O	2021
336	0340	Agrodyke	12%N: 18%P2O5: 12%K2O	2021
337	0341	FarmGrow Flowering and Fruiting Vegetative	5%N: 5%P2O5: 45%K2O + TE	2021
338	0342	Veggie Oemff Grow	14.8%N: 8.87%P2O5: 15.86%K2O + 1.93% S	2021
339	0343	Agribooster	19%N: 10%P2O5: 8%K2O	2021
340	0344	Eco Super Grow	15%N: 4.4%P2O5: 1.8%K2O	2021
341	0345	N P K 10:18:24	10%N: 18%P: 24%K: +0.5%Mg, 7%S, 0.012%Bo, 3%Xca	2021
342	0346	Maxiforce	20%N: 20%P: 20%K + 100ppm Zn, 800ppm Fe, 140ppm Cu,150ppm Mn	2021
343	0347	CynkMI	16.2%Zn	2021
344	0348	MI6.1	2.9%N	2021
345	0349	New Victory Flower and Fruit	17%N:14%P:34%K +0.03%B, 0.06%Zn,0.01%Fe,0.05%Cu, 0.05%Mn, 0.001%Mo, 0.007%Amino Acid	2021
346	0351	Calcium Nitrate		2017
347	0352	Polycoffee	19%N: 19%P2O5: 19%K2O	2017
348	0353	MoMI	11%Mo	2021
349	0354	Wangle	1.50% 1-Dodecane Sulfonic acid sodium salts	Jul-21
350	0355	KEM FOLIAR FEED	14%N: 9%P: 5%K +2%Mg	Jul-21
351	0356	Kyno Plus S	40%N + 6%S	Jul-21
352	0357	Kara	6.98%N: 3.88%P: 13.96%K	Jul-21
353	0358	NPS B	19%N: %P205+ 6.24%S, 0.12%B	Sep-21
354	0359	Zinc Sulphate Monohydrate	33.5%Zn	Sept-2021
355	0360	Trimix	6.5%Ca: 0.05%B: 15%Fulvic acid	Sept-2021
356	0361	Farma Booster Foliar Spray	15%Na	Nov 2021
357	0362	Green Urea	35%N:1%P:1%K	Dec-2021
359	0363	Micro p-topdressing	46%N: 0.1%Zn	Dec-2021
360	0364	Yaramila Otesha	13%N:24%P_2O_5:12%K_2O: 3%S: 2%MgO	Dec-2021
361	0365	Microp -planting	17%N:29%P_2O_5: 6%K_2O: 0.5%S:0.2%Zn	Dec-2021

362	0366	Durasop NPK Compound	22%N:6% P:12%K	Dec-2021
363	0367	Amcolon*K	7%N:7%P:40%K+ 1%MgO	Dec-2021
364	0368	DURASOP	12%N:12%P:17%K	Dec-2021
365	0369	Multiphos	10%N :25%P	Dec-2021
366	0370	AmcoCal Nit	15.5%N: 26% CaO	Dec-2021
367	0371	Amco SOP	50%K_2O:17.5%S	Dec-2021
368	0372	Amco PotaNit	13%N:46%K	Dec-2021
369	0373	Super cal 45	45%CaO	Dec-2021
370	0374	NutrOshield	10.2%N:0.2%B:1%Cu:0.02%Mn :4%Zn	Dec-2021
371	0375	ZAP	8%N: 1%S: 0.05%Mn: 0.05%Zn:0.10%Fe.	Dec-2021
372	0376	BorMI	12.1%B	Dec-2021
373	0377	nanoMI-Cu	14.5%N	Dec-2021
374	0378	MI ZBOZE	2.6%Mn	Dec-2021
375	0379	WapnMI nAgCu	18.5%CaO	Dec-2021
376	0380	KAL Booster	9.8%N:21%P:36.7%K:1.9%Mn:0.7% Fe:0.7%B:1.1%Zn:1.9%Cu:2.5%Mo	Dec-2021
377	0381	Yaramila Otesha	13%N:24%P2O5:10%K2O	Jan-2022
378	0382	Biophosphate	1.1%N: 39.6%P_2O_5: 0.11%K_2O.	Feb-22
379	0383	Microp Mbogamboga	15%N: 9%P_2O_5: 20%K_2O + 8.5%S, 0.02%B, 0.06%Zn	Feb-22
380	0384	MicroMI	1.38%Zn: 1.37%Fe: 1.67%Mn	Feb-22
381	0385	MI6	3%N:	Feb-22
382	0386	NanoMI	15.2%N:	Feb-22
383	0387	Energy Mix	11.2%N: 10.2%P: 11.8%K	Feb-22
384	0388	Veggie OEMFF Starter	14.80%N, 20.40%P205,18.80%K20, 1.9%S,1.30%Mg,0.12%Zn,0.14%B, 0.7%Fe,0.14%Mn,0.023%Cu,0.02%Mo	Feb-22
385	0389	KYNOCH PANDA PLUS	12%N: 46%P_2O_5 + 5%S, O.5%Zn	Mar-22
386	0390	Master Winner	15%N: 3%P_2O_5: 5%K_2O + 0.3%MgO, 20%S	Mar-22
387	0391	DURAMON 30	30%N: 0%P: 1%K +2.5%MgO, 18.5%SO3	Mar-22
388	0392	Star Farm Booster	16.98%N: 8.9%P_2O_5: 12.35%K_2O.	Apr-22
389	0393	AGROGOLD NPK	3.98%N: 3.6%P_2O_5 : 2.4%K_2O	Apr-22
390	0394	EXCELLENT SUPER	24%N: 24%P_2O_5: 18%K_2O + 0.9%MgO	Apr-22
391	0395	LIQUID SEAWEED PLANT GROWTH PROMOTER	50.5 mg/L N: 9.70mg/L P: 1670mg/L K + 0.83mg/L Mg	May-22
392	0396	HCPS	0.9%N: 0.43%P_2O_5: 3.25%K_2O + 0.45%Ca, 1.04%Mg	May-22
393	0397	GEM SUPER K	18.3%N: 21.4%P_2O_5: 41.6%K_2O	May-22
394	0398	Biostimulant	0.65%N: 45% K_2O	May-22
395	0399	Power grower max-Vegetative	25.2%N: 22.7% P:17.5% K	May-22
396	0400	Power grower max K	9.9%N: 21.5% P: 44.7% K	May-22
397	0401	YUKON (K)	26.6%K_2O + < 0.3 %Cl	June-22
398	0402	BACK (K)	47.4%K_2O + < 0.15%Cl	
399	0403	MAIZE - PLUS	140g/L N: 60g/L P + 470mg/L B, 684mg/L Zn, 1005g/L Fe, 510mg/L Cu, 510g/L Mn, 59mg/L Mo	June-22
400	0406	SUBA AGRO FOLIAR	23 %N: 23 %P: 23 %K + 0.01 %B, 0.01 %Zn, 0.05 %Fe, 0.0006 %Cu, 0.03 %Mn, 0.004 %Mo.	June-22
401	0407	BOOSTER EXTRA SUPER K	23 %N: 4 %P: 36 %K	June-22
402	0408	BIO - GENIC FERTILIZER	31 %K + 17.5 %Ca, 52.81 %S, 0.5 %Zn, 2.1%Fe, 0.03 %Cu	June-22

Kilosa washangilia ujenzi wa kiwanda cha mbolea Dodoma

• Mkuu wa Wilaya awataka kuchangamkia soko la samadi

Na **MWANDISHI WETU**

Wananchi wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, wametakiwa kuchangamkia fursa zitakazoletwa na kiwanda cha mbolea cha Itracom Fertiliser Limited kinachojengwa jijini Dodoma ambacho kitazalisha mbolea ya mchanganyiko wa samadi na kemikali kwa uwiano sawa.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga, amesema kwamba kwa kuwa mbolea itakayozalishwa kwenye kiwanda hicho itakuwa na mchanganyiko wa samadi na kemikali kwa uwiano sawa itafungua fursa kwa wafugaji kukusanya samadi inayotokana na kinyesi cha mifugo na kukiuzia kiwanda hicho na hivyo kupata soko la uhakika la samadi.

Bw. Mwanga alisifu diplomasia ya uchumi ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumpata mwekezaji wa kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited na akasisitiza kwamba ni kiongozi mwenye maono asiyependa kuzungumza bila vitendo.

Mkuu huyo wa wilaya aliyasema hayo katikati ya mwezi Mei mwaka huu alipokuwa mgeni rasmi wakati wa hafla ya kuelimisha wakulima wa eneo la Ilonga kuhusu namna mbolea itakayozalishwa na kiwanda hicho inavyofanya kazi katika kuongeza tija kwenye kilimo.

"Samadi sasa hivi ni mali. Tutapata zabuni ya kukusanya samadi na kupeleka kiwandani ili kutumika kama malighafi ya kutengenezea mbolea itakayotumiwa na mkulima na kumwezesha kupata mavuno mengi atakayouza ndani na nje ya nchi na kuingizia pesa za kigeni," Mwanga alisema

Kupitia mashamba darasa yaliyopandwa kwa kutumia mbolea itakayokuwa ikizalishwa na kiwanda hicho inayojulikana kama fomi pandia, fomi kuzia pamoja na mbolea iliyozoeleka na wakulima wengi nchini aina ya DAP na Urea zimetumika katika mashamba darasa yaliyopo katika skimu ya umwagiliaji wa zao la mpunga katika kijiji cha Ilonga,kata ya Chanzulu, wilayani Kilosa, ili kuonesha utendaji wa mbolea hizo na kuwafanya wakulima wachague mbolea itakayowafaa kwenye kilimo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dkt. Geoffrey Mkamilo alisema taifa lina matumaini makubwa na mbolea itakayozalishwa na Itracom Fertilizer Limited katika kutatua changamoto ya upatikanaji na bei ya mbolea nchini.

Hata hivyo, Mkamilo alisema TARI inaendelea na utafiti wa kuona utendaji wa mbolea hiyo ambapo inaangalia ulinganifu wa kiasi kinachowekwa kwenye mazao na matokeo yake na baadaye kuwaeleza wananchi matokeo ya utafiti huo.

Alisema, pamoja na kujaribu mbolea hiyo katika eneo hilo, TARI inafanya utafiti kama huo katika maeneo mengine nchini ambayo ni Hombolo, Seriani mkoani Arusha na Uyole mkoani Mbeya.

"Tumeanza kufanyia majaribio ya mbolea hapa Ilonga kwa zao la mpunga, zao la alizeti na mtama Homboro, zao la maharage na mahindi eneo la Seriani mkoani Arusha na mkoani Mbeya kwa zao la mahindi, maharage, viazi na mpunga," alisema Dkt. Mkamilo.

TARI pia inaendelea na zoezi la kupima afya ya udongo nchi nzima na tayari mikoa 18 imeshapimwa na kwamba wanaendelea kukamilisha kwa mikoa 8 iliyosalia ili kufahamu udongo una rutuba ya kiasi gani na umepungikiwa na virutubisho gani ukilinganisha na mahitaji ya zao husika.

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo, alipongeza hatua ya ujenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited na kusema kujengwa kwa kiwanda hicho nchini kutatatua changamoto ya upatikanaji na bei ya mbolea kwa wakulima.

Aliongeza kuwa ujenzi wa kiwanda umetokana na utashi wa kisiasa wa viongozi wa juu nchini na kutoa wito kwa wawekezaji wengine kuja kuwekeza katika tasnia ya mbolea huku akibainisha uwepo wa malighafi kwa ajili ya kutumika kwenye viwanda vya mbolea.

"Malighafi kwa ajili ya kutengeneza mbolea zipo na zinapatikana kwa wingi nchini, nishati ya uhakika ipo, nguvu kazi ipo na soko lipo hivyo karibuni kuwekeza," Dkt Ngailo alisisitiza.

Pamoja na hayo aliwataka waingizaji, wazalishaji na wauzaji wa mbolea nchini kujisajili kwenye mfumo wa ruzuku ili waweze kushiriki kwenye biashara ya mbolea ya ruzuku kwa wakulima.

Mkurugenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited, Nduwimana Nazaire aliwahakikishia wakulima wa Ilonga na Tanzania kwa ujumla upatikanaji wa uhakika wa mbolea na kubainisha kuwa bei ya mbolea itakayozalishwa kiwandani hapo itakuwa nzuri ukilinganisha na aina nyingine za mbolea zinazoingizwa nchini.

"Napenda kuihakikishia serikali na wakulima kwa ujumla wasiwe na mashaka mbolea itapatikana na itakapotosheleza mahitaji ya ndani ndipo tutaisafirisha kwenda nje ya nchi," Nazaire alisema.

Mkulima mmoja, ambaye shamba lake limetumika kuonesha matokeo ya mbolea zilizokuwa zikijaribiwa kwenye mashamba darasa, aliishukuru TARI kwa kupeleka mradi huo katika kijiji chao na kukiri mbolea ni kilio cha wakulima wa eneo la Kilosa.

Alisema wakulima wa Kilosa wamefurahia sana ujio wa kiwanda hicho nchini huku wakiamini watakuwa wanufaika wa kwanza kwa kupata bidhaa hiyo adhimu itakayowasaidia kuongeza tija katika kilimo.

Ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha ITRACOM Limited unaendelea eneo la Nala jijini Dodoma

Jarida hili hutolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)
Mtaa wa Kilimo, Jengo la Kilimo I Complex, Barabara ya Mandela,
S.L.P. 46238 Dar es Salaam. Simu. +255 22 2861939 Tovuti: www.tfra.go.tz